**Mfugaji** adaiwa kumpiga risasi mkulima kisa mifugo kuingia shambani

UKURASA 3



**Samia** amlilia mwanzilishi Precision Air

UKURASA 2




UKURASA 9


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

JUMAPILI

Jumapili Juni 11, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581338

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


## Wanandoa vikongwe walilia fidia nyumba kubomolewa

UK 8



# Kanisa lilivyobambwa na tiba kwa maombi

• **Lina** wodi za nyasi na udongo, wagonjwa marufuku kwenda hospitalini... *Endelea Ukurasa wa 2*








Baadhi ya nyumba za nyasi na udongo zinazotumika kama wodi za wagonjwa katika Kanisa la Maombezi la Lulembo, Misungwi mkoani Mwanza, zinazodaiwa kujengwa na waumini wanaofika na wagonjwa wao kwa maombezi. **PICHA NDOGO**: Maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama wakishirikiana kuwaondoa waumini na wagonjwa kanisani hapo baada ya agizo la Mkuu wa wilaya hiyo, Paulo Chacha (hayuko pichani) la kufungwa kwa kanisa. **PICHA ZOTE: VITUS AUDAX**

# Vuta nikuvute Spika, Mdee Azimio uendeshaji bandari





UKURASA 2

**MICHEZO** **MAPOKEZI YA YANGA BALAA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Kanisa lilivyobambwa kwa tiba maombi

**Na Vitus Audax,** MISUNGWI

WAKATI sintofahamu ya Kanisa la Kenya lililowataka waumini wake kuishi kwa kufunga bila kula na kusababisha zaidi ya vifo 90 halijatoweka vichwani mwa watu, kanisa lingine limebainika wilayani Misungwi mkoani Mwanza, likikusanya wagonjwa na kuwazuia kwenda hospitalini.

Nchini Kenya, miili ya watu 95 ilifukuliwa kwenye makaburi ya jumla kwenye msitu wa Shakahola baada ya kiongozi wa wa kanisa moja, Paul Mackenzie Nthenge, akidaiwa kuwahubiria waumini wake kwamba kukaa na njaa ndiyo njia pekee ya kwenda kwa Mungu.

Wakati jambo hilo likiwa chini ya uchunguzi nchini humo, kanisa lingine lijulikanalo kwa jina la Lulembo linalomilikiwa na Mzee Wiliam Luboja, lenye zaidi ya waumini 200, ndani yake kukiwa na zaidi ya wodi bubu 100 zilizojengwa kwa udongo na kuezekwa kwa nyasi labainika Tanzania.

Inadaiwa kuwa, mzee huyo amekuwa akiendesha kazi hiyo kwa kuwakusanya wagonjwa na kuwafikisha katika kanisa hilo huku kibali chake kikiwa ni kuendesha shughuli za tiba asili.

Kutokana na sintofahamu hiyo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Paulo Chacha, ameliagiza Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kutosha katika eneo hilo ili kubaini endapo kuna makaburi ya watu wanaofariki dunia kutokana na maombezi hayo.

Pia amelitaka jeshi hilo kuwahoji wamiliki na viongozi wa kanisa hilo ili kufahamu namna wanavyoziendesha shughuli zao bila kibali.

"Yawezekana wazee hawa wanaendesha shughuli za matibabu ya asili lakini ni tofauti na kinachoendelea hapa maana haiwezekani tiba ifanyike kwa maombi na eneo hili lina wodi bubu zaidi ya 100.

"Kwa nini wasiende kutibiwa hospitalini na tukiangalia kwa makini hapa lazima tutakutana na makaburi," alisema. Kiongozi huyo alisema wagonjwa wote walioko katika eneo hilo,watawapeleka katika vituo vya afya na wote waliohusika watakamatwa.

"Hapa hatobaki mgonjwa yeyote na watu wote hao tunawakamata na matumizi ya kanisa hilo yafungwe kwani halina vibali vya kuendeshwa hapa," alisema Chacha.

Mmiliki wa kanisa hilo, Mzee Luboja, alisema alianza shughuli hizo baada ya kupokea maono ya kutibu kupitia maombi wala si kwa tiba asili kama kibali chake cha kazi kinavyoeleza.

"Niliendа kupata tiba ya namna hii na baada ya kupona nikaambiwa kuwa na mimi nina karama ya namna hii, hivyo naweza kwenda na kuanza kuponya watu kwa njia ya maombezi si ya kimila wala si ya dini (anaitaja)," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo (kushoto), akikagua uchimbaji wa madini unavyoharibu maji ya Mto Mbwemkuru ambao ni chanzo cha maji safi na salama kwa zaidi ya wananchi 1,000 wilayani humo, juzi. Wengine ni Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Nachingwea, Mhandisi Sultan Ndoliwa (wa pili kushoto) na viongozi mbalimbali. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Vuta nikuvute Spika, Mdee Azimio uendeshaji bandari

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

MVUTANO wa kisheria baina ya Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee, na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, uliibuka jana bungeni wakati wabunge wakichangia hoja ya serikali kuhusu mkataba wa makubaliano kati ya serikali ya Tanzania na Dubai.

Mkataba huo ni unaohusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa bandari Tanzania. Wakati Mdee akichangia suala hilo, alijikuta akikatishwa mara kwa mara na wabunge wenzake.

Katika mchango wake, Mdee alionyesha wasiwasi kuhusu mkataba huo kwa kunukuu Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwamba makubaliano yaliyofikiwa kati ya serikali na kampuni ya DP World yanaweka msingi wa kisheria na si mkataba wa makubaliano.

"Tunaambiwa makubaliano yanaweka msingi wa kisheria na si mkataba na sisi ndio tunazungumza hapa kama msingi una mashaka, una matobo, kama msingi hauna maslahi ya kitaifa. Huo mkataba wanaosema tutaletewa hapa bungeni lazima uendane na hii sheria hapa," alisema Mdee.

Pia alisema sehemu ya kwanza ya makubaliano hayo inahusisha magati ambayo Tanzania ilikopa takribani Sh. trilioni moja kwa ajili ya urekebishaji.

Baada ya kauli hiyo, Spika alimsimamisha na kumwambia amweleweshe kuwa serikali inaipa DP WORLD hilo ambalo imewekeza Sh. trilioni moja ili afanye nini kwa mujibu wa vifungu alivyokuwa anarejea.

"Mimi nisaidie jambo moja kwenye lile eneo ambalo fedha zimetumika za Mtanzania. Sehemu ya kwanza inasema maendeleo, usimamizi na uendeshaji. Huku mwanzoni inasema wigo wa makubaliano haya ni kuwezesha utekelezaji wa maeneo ya ushirikiano kiambatisho cha kwanza cha makubaliano haya, kama hivyo ndivyo ... kwa nini usifikiri lile eneo linakwenda kwenye opereshеni? Baada ya swali hilo, ndipo Mdee aliposema hawezi kuiongelea serikali, kitendo ambacho Spika alifafanua kwamba mkataba huo haujaweka msingi wa maeneo ambayo yatafanyiwa kazi bali umetaja maeneo yenye uwezekano wa kufanyiwa kazi.

Spika alisema ndiyo maana azimio limepelekwa bungeni ili wabunge watoe maoni yao na serikali ikayaangalie inapokwenda kutia saini mkataba.

Mdee akiendelea kuchangia, alisema awamu ya pili ya mkataba huo inahusisha kuendeleza, kusimamia na kuendesha, majukumu ambayo kwa mujibu wa Sheria ya Bandari ya mwaka 2014 na marekebisho yake ya mwaka 2019, ni majukumu ya bandari. "Kama nia ni njema, kwa nini aspect ya PPP (ubia kati ya sekta binafsi na ya umma) isionekane kwenye makubaliano yanayokuja kuwa sheria ya kimataifa? Makubaliano haya, bandari ni mwezeshaji tu wa mazungumzo, hata umiliki wa ardhi bandari hajulikani yuko wapi?" alihoji.

Mbunge huyo alisema mkataba huo haujaweka mawanda ya bandari zitakazotumika kwa kuzitaja bandari husika kuwa Tanzania ina bandari takribani 69 zinazotambulika kisheria kwenye Bahari ya Hindi na maziwa, jambo ambalo Spika alisema halijatajwa kwenye mkataba, hivyo mbunge huyo anakisia jambo ambalo si sahihi.

Kitendo hicho kilimlazimu Spika kurejea Kanuni ya Bunge na kusema: "Waheshimiwa wabunge tuelewane vizuri. Kanuni yetu ya 111 inasema hivi, majadiliano wakati wa kujadili hoja ya kuridhia mkataba yatahusu masharti ya mkataba husika.

"Kwa hiyo hakuna mkataba nje ya haya unaoweza kuzungumziwa kwenye ngazi hii kwa hiyo nimwelewe yeye (Mdee) anasema anaona mbali kwa hiyo anatoa maoni yake. Kwa hiyo Waheshimiwa myasikilize upande wa serikali."

# Samia amlilia mwanzilishi, Mwenyekiti Precision Air

**Na Halfani Chusi**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemlilia mwanzilishi na Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Precision Air Tanzania, Michael Shirima, aliyefariki dunia usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Aga Khan jijini Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu.

Katika ukurasa wake wa Twitter jana, Rais Samia alisema Shirima alikuwa na mchango mkubwa katika sekta ya usafiri wa anga.

"Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Michael Ngaleku Shirima, Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Precision Air Tanzania.

"Baada ya utumishi wake kwa umma kwa takribani miaka 30, amekuwa sehemu muhimu katika biashara ya anga na shughuli za kijamii katika nchi yetu," aliandika Rais Samia.

**RATIBA MAZIKO**

Akizungumza kwa niaba ya msemaji wa familia nyumbani kwa mtoto wa marehemu, Meneja Masoko wa Precision Air, Hilali Mremi, alisema Shirima alifariki dunia saa 3:00 usiku na kwamba ratiba kamili ya maziko itatolewa leo saa 4:00 asubuhi na msemaji wa familia.

Alisema Shirima alikuwa mtu mwenye upendo na busara na kwamba pengo lake halitazibika.

"Shirima alikuwa mshauri kwa wafanyakazi. Alipenda kuona kila mtu anafanikiwa, alikuwa mtu mwenye busara na alipenda ushirikiano," alisema.

Shirima amewahi kufanya kazi katika Shirika la Ndege la Tanzania na katika upambanaji wa kutafuta maisha, amewahi kufanya biashara ya kuchoma nyama na kuendesha malori ya kwenda Mwanza mpaka alipoanzisha shirika la ndege.

Pia wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro alikotokea, alianzisha kituo cha watoto yatima na kwamba hivi karibu alikuwa anajenga zahanati kwa ajili ya watoto yatima.

Precision Air ilianzishwa mnamo 1991 na kuanza kutoa huduma mwaka 1994. Hapo awali, kampuni hii ilikuwa ya binafsi lakini Kenya Airways iliinunua asilimia 49.

Licha ya kuwa mwanzilishi wa Precision Air, Shirima pia alikuwa anamiliki asilimia tano za hisa katika benki ya I&M Tanzania ambayo hadi kufikia Desemba, 2021 ilikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 130 sawa na Sh. bilioni 200. Pia alikuwa mjumbe wa bodi ya wakurugenzi.

Aidha, Shirima aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya kampuni ya TOL Gases Limited ambayo inazalisha gesi za hospitalini na viwandani.

**HABARI KITAIFA**

# Bunge laridhia Azimio mkataba ushirikiano uendeshaji bandari

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

BUNGE limepitisha Azimio la pendekezo la kuridhiwa kwa mkataba baina ya serikali ya Tanzania na Dubai unaolenga ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji utendaji kazi wa bandari.

Akitoa maelezo kuhusu mkataba huo jana bungeni jijini hapa, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alitaja faida 14 zitakazopatikana kupitia ushirikiano huo. Mbarawa alisisitiza kuwa, utapunguza muda wa meli kukaa nangani kutoka siku tano za sasa mpaka saa 24, hivyo kuongeza idadi ya meli katika bandari ya Dar es Salaam kutoka meli 1,569 zilizohudumiwa mwaka 2021/22 mpaka 2,950 ifikapo mwaka 2032/33.

Nyingine ni kupunguza muda wa ushushaji wa makontena kutoka siku nne na nusu mpaka siku mbili, kupunguza muda wa uondoshaji mizigo kutoka saa 12 mpaka saa moja kutokana na uboreshaji wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Kadhalika kupunguza gharama ya usafirishaji wa mizigo kutoka nchi za nje kwenda nchi za jirani. "Kwa mfano kutoka Dola 12,000 mpaka kati ya Dola 6,000 na Dola 7,000 kwa kasha linalokwenda Malawi, Zambia au DRC. Hii italeta watumiaji wengi kwenye Bandari ya Dar es Salaam," alisema.

Faida nyingine alizitaja ni kuongezeka kwa shehena inayohudumiwa kutoka tani milioni 18.41 za mwaka 2021/22 hadi kufikia tani milioni 47.57 mwaka 2032/33, sawa na ongezeko la asilimia 158 pamoja na kuongezeka kwa mapato ya serikali yatokanayo na kodi ya forodha inayokusanywa katika shehena inayopitishwa bandarini kutoka Sh. trilioni 7.76 za mwaka 2021/22 hadi Sh. trilioni 26.7 za mwaka 2032/33, sawa na ongezeko la asilimia 244.

Alitaja faida nyingine kuwa ni kuongezeka ajira zinazotokana na shughuli za bandari kutoka 28,990 mwaka 2021/22 hadi ajira 71,907 ifikapo mwaka 2032/33, sawa na ongezeko la asilimia 148.

"Kuboresha maeneo ya kuhudumia shehena ya makasha na kuweka mitambo yenye teknolojia ya kisasa na kuendeleza eneo la kuhifadhia mizigo la bandari kavu kwa kuweka miundombinu ya kisasa ya kuhudumia aina zote za shehena.

"Kuboresha magati ya kuhudumia majahazi na abiria ikiwa ni pamoja na kushawishi uingiaji wa meli kubwa za kitalii zitakazoongeza idadi ya watalii nchini na kuongeza pato la taifa, kusimika mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya shughuli za bandari na kuwaunganisha wadau wake, kutolewa mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa TPA katika Bandari zote," alisema.

Mbarawa alisema kutakuwa na uanzishwaji wa maeneo maalum ya kiuchumi na viwanda; na kuchochea ukuaji wa sekta zingine za kiuchumi zikiwamo sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi; kuchagiza shughuli za viwanda na biashara na kuchagiza ukuaji wa sekta ndogo za usafirishaji kwa njia ya reli na 13 barabarani.

"Watanzania kunufaika na teknolojia na ujuzi wa uendeshaji wa bandari kisasa na kujenga uhusiano wa kidiplomasia," alisema.

Mbarawa alisema kunatoa haki ya upekee ya kufanya majadiliano kwa awamu ya miradi iliyoainishwa kwenye mkataba huo kwa kipindi kisichozidi miezi 12 ili kuwezesha pande mbili kufanya majadiliano.

"Hivyo iwapo kipindi hicho kitakwisha bila kufikia makubaliano, TPA inaweza kuanzisha majadiliano na wawekezaji wengine katika maeneo hayo pasipo kuwapo kwa mgogoro wowote chini ya mkataba huo," alisema.

Alisema kutokuwapo kwa ufanisi katika bandari hiyo kumesababisha athari mbalimbali ikiwamo meli kusubiri muda mrefu nangani hali inayochochea kuongezeka kwa gharama ya kutumia bandari ya Dar es Salaam.

"Kwa mfano gharama za meli kusubiri nangani kwa siku moja ni takriban Dola za Marekani 25,000, sawa na takriban Shilingi milioni 58 kwa siku, meli kutumia muda mrefu kupakia na kupakua shehena gatini kwa wastani wa siku 5 ikilinganishwa na siku moja inayokubalika kimataifa; meli kubwa kutokuja katika bandari ya Dar es Salaam kutokana na kuchukua muda mrefu kuhudumiwa," alisema.

Alisema athari hizo zimesababisha bandari hiyo kuwa inayolishwa shehena na bandari zingine hivyo kuongeza gharama ya kuitumia na kuikosesha nchi mapato ambayo yangeweza kutumika katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo ingesaidia kukuza uchumi na kuboresha huduma za wananchi

Waziri Mbarawa alisema ufanisi huo mdogo umetokana na changamoto mbalimbali zikiwamo, kukosekana kwa mifumo ya kisasa ya TEHAMA, kutokuwapo kwa maeneo ya kutosha ndani na nje ya bandari kwa ajili ya kuhifadhia shehena pamoja na maegesho ya meli.

Pia alisema kukosekana kwa mitambo ya kutosha na ya kisasa ya kuhudumia shehena ambayo teknolojia yake inabadilika mara kwa mara na ina gharama kubwa ya uwekezaji na uendeshaji.

Alisema uendeshaji huo hauna masharti yanayoifunga serikali kuhusu maeneo ya ushirikiano yaliyoainishwa pasipo uwapo wa mkataba mahsusi wa utekelezaji wa miradi itayojadiliwa na kukubaliwa na pande mbili kwa kuwa lengo lake ni kuweka msingi wa ushirikiano baina ya serikali mbili kwa maeneo mahsusi yaliyoainishwa ndani ya mkataba wa IGA kama taasisi tekelezi ambazo ni TPA na DP World.

Alisema uwekezaji chini ya mkataba huo hautahusisha uendelezaji na uendeshaji wa bandari yote, bali mikataba mahsusi ya miradi ambayo itajadiliwa na kuingiwa kwa kila eneo la ushirikiano na itahusisha matumizi ya ardhi pekee na sio umiliki wa ardhi ikiwa ni pamoja na serikali kuhakikisha kuwa Sheria, kanuni na taratibu zinasimamiwa ipasavyo.

# Mfugaji adaiwa kumpiga risasi mkulima mifugo kuingia shambani

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

MKULIMA Walter Kaaya (34) mkazi wa wilayani hapa, amenusurika kifo kwa madai ya kupigwa risasi ya bega na mfugaji Paulo Sipiteki (43), kutokana na mzozo kati yao kuibuka baada ya ng'ombe kuingia shambani na kuharibu mazao.

Inadaiwa mfugaji huyo ambaye ni mkazi wa Arusha, alichukua uamuzi wa kumpiga risasi mkulima huyo mwenye shamba la ekari 200 baada ya mifugo kuharibu mahindi na maharage shambani hapo.

Wakati Kaaya akiwaondoa ng'ombe hao ili kuepusha uharibifu kwenye shamba lake ndipo kukatokea mzozo huo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) George Katabazi, akizungumza kwa njia ya simu na mwandishi wa Habari hii jana, alisema tukio hilo lilitokea Mei 24, mwaka huu, na kwamba mtuhumiwa huyo alikamatwa siku saba baadaye.

Alisema wakati mkulima huyo akiondoa mifugo shambani, mtuhumiwa alifika na kuibua mzozo na kuchukua silaha yake aina ya bastola yenye risasi tano na kumpiga risasi mwenzake eneo la begani.

"Majeruhi alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC Moshi, mkoani Kilimanjaro kwa matibabu na baada ya tukio mtuhumiwa huyo alitoroka," alisema.

Alisema baada ya tukio hilo jitihada za kumsaka zilianza na kukamatwa akiwa amejificha katika Kijiji cha Nyumba ya Mungu. "Kitendo alichofanya mtuhumiwa alijichukulia sheria mkononi badala ya kufuata sheria kwa kuripoti kituo cha polisi au kwa viongozi wa serikali za vijiji. Uamuzi wa kujichukulia sheria mikononi haukuwa na sababu yoyote ya kumjeruhi mtu, badala yake angetumia taratibu,"alisema.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**COLIN MICHAEL BEALE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya LANDROVER yenye usajili namba **T389 AQB,** CHASSIS NAMBA: SALL-**DHMF7TA973458** na ENGINE NAMBA: **16L29324A**. kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/197265/2023**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MABULA BEATUS LUSHINGE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 920 DGY** aina ya **TOYOTA RAV 4**. Chassis namba **OSXA110005328.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/197575/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
09.06.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe 12.06.2023 hadi 18.06.2023 kampuni ya **CEVA Interfreight Tanzania** itasafirisha Gari mbili (2) Tupu zenye vipimo vikubwa kutoka Mzenga kuelekea Bandari ya Dar es salaam , gari hizo zenye namba za usajili: **NRB97300/NRB15200 DS00TG-GP/NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **36.5** |
| **Mita Upana** | - | **4.3** |
| **Mita Kimo** | - | **4.6 Mita** |

3. Njia itakayotumika: **BARABARA YA MOROGORO na BARABARA YA MANDELA hadi BANDARI YA DAR ES SALAAM** kupitia **MLANDIZI,** gari litasafiri muda wa mchana tu. ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

Ndugu **PHILEMON REVELIAN KASEIJA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Fuso lenye namba za usajili **T642 DKM.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/197304/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI, MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......54/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: SALVATORY SAMWEL WA MAZIMBU**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: SYLVANUS SAMWEL NA FAUSTINE SAMWEL**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 12 Mwezi 06 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 09 mwezi 06 mwaka 2023**

G.A. NG'ITU
HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## Mikoa sita yakabidhiwa magari ya maji na usafi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Afya imekabidhi magari sita yenye thamani ya Sh. milioni 500 kwa ajili ya kusaidia shughuli za maji na usafi wa mazingira katika mikoa ya Shinyanga, Lindi, Simiyu, Katavi, Singida na Ruvuma.

Magari hayo yalikabidhiwa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekalaghe, jijini hapa katika hafla iliyohudhuriwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga aliyewawakilisha Makatibu tawala wengine pamoja na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Kheri Kagya.

Dk. Shekalaghe alisema hii ni awamu ya pili ya utoaji wa magari hayo. Awamu ya kwanza yalitolewa mengine sita na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kuyatoa kwa ajili ya uratibu wa shughuli za maji na usafi wa mazingira utakaosaidia kukabiliana na magonjwa mbalimbali kwa wananchi.

Kiongozi huyo ametoa wito kwa wananchi kuweka jitihada za kusafisha mazingira na kutunza vyanzo vya maji ili kuepuka magonjwa hasa ya mlipuko yakiwamo kipindupindu na homa ya matumbo ambayo husababishwa na uchafuzi wa mazingira.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Prof. Siza Tumbo, alisema licha ya mkoa wake kuendelea kufanya vizuri kwenye usafi wa mazingira, gari hilo litasaidia kuongeza kasi zaidi ya utoaji elimu.

Mratibu wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Wizara ya Afya, Anyitike Mwakitalime, alisema mradi wa huduma endelevu za maji na usafi wa mazingira unatekelezwa katika mikoa 17 na halmashauri 86 na mpaka sasa, ujenzi na matumizi ya vyoo bora umefikia asilimia 74 ya kaya zenye vyoo bora.




Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Ilala, Fratha Katumwa (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Diwani wa Kata ya Kisukuru, Lucy Lugome iliyotolewa na wanachama wa chama hicho, alipokuwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa ilani ya CCM katika kata hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Katibu wa CCM wa kata hiyo, Menasi Mbele. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# CWT: Kikao kilichomng'oa katibu mkuu batili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimekemea kitendo cha Naibu Katibu Mkuu wake, Mwalimu Joseph Msalaba, na kaimu Mweka Hazina Taifa, Mwalimu Protas Magesa, na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Utendaji kuvunja katiba na kanuni za chama hicho kwa maslahi binafsi.

Rais wa CWT, Leah Ulaya, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa tamko kwa vyombo vya habari kuhusu viongozi hao na baadhi ya wajumbe wa kamati ya utendaji waliofanya kikao na kutoa maazimio ya kumsimamisha Katibu Mkuu, Japhet Maganga, kutojihusha na shughuli zote za chama.

"Juni 6, 2023 baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa walikusanyika katika viunga vya ofisi ya CWT makao makuu katika kile walichokiita kikao cha dharura cha Kamati ya Utendaji ya CWT na vyombo vya habari vilialikwa na kutoa taarifa kwa umma juu ya maazimio ya kikao hicho.

"Kikao hicho kilizua taharuki kwa wanachama, wadau na umma kwa ujumla, hivyo uongozi wa chama unatoa ufafanuzi na tamko juu ya sakata hilo," alisema Ulaya.

Alisema kikao kilichofanyika na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa chini ya Uenyekiti wa Mwalimu Thobias Sanga mjumbe kutoka mkoa wa Njombe na Katibu wake, Joseph Msalaba, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu ni kinyume cha Ibara ya 21.3(c) ya Katiba ya CWT.

"Ni kinyume cha Katiba ya CWT toleo la sita la mwaka 2014 pamoja na Kanuni ya 5 (b) ya Kanuni za CWT Toleo la Nne la mwaka 2015. Rais wa CWT ambaye ni mwenyekiti na katibu mkuu CWT ambaye ndiye katibu wa vikao vya chama ngazi ya taifa ndio wenye uhalali wa kuitisha vikao," alisema.

Pia alisema kitendo cha mwenyekiti na katibu wa kikao hicho batili cha Kamati ya Utendaji Taifa kutoa taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari ni kupoka mamlaka na madaraka ya Rais wa CWT kinyume cha Ibara ya 23 (23.1) (c) ya Katiba ya CWT Toleo la Sita la mwaka 2014.

"Ili kuondoa sintofahamu iliyotokana na kikao batili cha Juni 6 pamoja na maazimio yake, Msajili wa Vyama vya wWfanyakazi na Waajiri kupitia barua Kumb. Na.DA 27/380/12/21 ya Juni 9 , 2023 kwa Katibu Mkuu wa CWT amebatilisha maazimio ya kikao hicho na utekelezaji wake kwa kuwa hakikuwa halali na maamuzi yake yalikuwa batili hayakuzingatia katiba na kanuni za CWT," alisema.

Kadhalika, alisema kutokana hali hiyo, uongozi wa CWT Taifa unawataka wadau, wanachama na umma kwa ujumla, wapuuze maazimio ya kikao hicho haramu kilichofanyika kwa nia ovu.

"Wanachama, watumishi viongozi wote wa CWT na wadau waendelee kupokea taarifa za kiutendaji za chama kutoka kwa Mwalimu Japhet Maganga ambaye ndiye katibu mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania aliyechaguliwa na mkutano mkuu halali wa CWT," alisema.

Ulaya aliwataka wanachama na wadau wote kuwa na subira wakati chama kinaendelea kuchukua hatua stahiki za kinidhamu kwa wote walioshiriki kuvunja Katiba na Kanuni za CWT kwa makusudi.

# Majaji tuzo za EJAT 2022 waanza kazi

**Na Halfani Chusi**

JOPO la majaji saba limeanza mchakato wa kuwatafuta washindi wa Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa mwaka 2022, baada ya kuapishwa na Jaji Robert Makaramba, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Katika tuzo hizo, Kampuni ya The Guardian waandishi wake wamepeleka kazi 43 kwa magazeti ya Nipashe na The Guardian.

Majaji hao wakiongozwa na mwandishi mkongwe Mkumbwa Ally, walianza jana kupitia jumla ya kazi 893 kutoka vyombo vya habari 60, huku mchakato huo ukipangwa kufanywa kwa siku nane mfululizo.

Akizungumza katika hafla ya kuwaapisha majaji hao, Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, alisema katika tuzo hizo, kazi zilizopokewa ili kushindanishwa katika vipengele 20. Mwaka jana jumla ya kazi 598 za EJAT 2021 zilipokewa.

Mukajanga alisema katika mashindano hayo, Dar es Salaam imetoa asilimia 21.8 sawa na waandishi 98 ikifuatiwa na Arusha asilimia 12.7 sawa na waandishi wa habari 57 na Pemba asilimia 12 sawa na waandishi wa habari 54. Katika kazi zilizopokewa, alisema wanawake ni 393 na wanaume 335.Alisema makundi ya kushindaniwa kwenye tuzo hizo yameongezwa kutoka 19 ya mwaka 2021 hadi 20.

Aliyataja makundi yaliyoongezwa ni Tuzo ya Uandishi wa Habari za Utunzaji wa Mazingira na Vyanzo vya Maji; Tuzo za Uandishi wa Habari za Kodi; Tuzo na Mapato; Tuzo za Uandishi wa Habari na Sensa na Tuzo ya Uandishi wa Habari za Afya ya Uzazi.


"Katika tuzo hizi kundi lililoongoza kuwa na kazi nyingi ni la habari za watoto na jinsia ambapo kazi 139 zilikusanywa. Kundi la afya ni kazi 110, kundi la wazi kazi 94, tuzo ya uandishi wa habari na utunzaji wa vyanzo vya maji kazi 63, na habari za kilimo na biashara,' alisema.

Alisema washindi watakaopatikana akiwamo yule wa tuzo ya mafanikio katika maisha ya uandishi wa habari, watakabidhiwa tuzo zao usiku wa Julai 22, mwaka huu, katika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Majaji watakaoendesha mchakato huo, mbali na Mkumbwa, ni Mwanzo Millinga, Dk. Egbert Mkoko, Rose Mwalimu, Mbaraka Islam, Peter Nyanje na Nasima Chum.

Baada ya hafla ya kuwaapisha majaji hao, Jaji Makaramba aliwataka watende haki kwa washindani na kumtanguliza Mungu wakati wa kumtafuta mshindi.

HABARI KITAIFA




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (watatu kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya sh. bilioni 14.82 kwa Mkurugenzi wa Fedha wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Beatrice Musa-Lupi (katikati), ambazo ni gawio kutoka Benki ya CRDB, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Diwani matatani madai kuhamasisha wananchi wasishiriki kwenye miradi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

DIWANI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Kata ya Mitundu Halmashauri ya Itigi wilayani hapa, Patrick Masanja, ameshitakiwa kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, na viongozi wa wilaya hiyo kuwa ni kikwazo cha utekelezaji wa miradi.

Viongozi hao wamedai kuwa, diwani huyo amekuwa akishawishi wananchi wagome kushiriki nguvu kazi katika kata hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemilembe Lwota, alimweleza Mkuu wa Mkoa juzi kwamba, diwani huyo kwa muda mrefu amekuwa akishawishi wananchi wasishiriki nguvu kazi kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa na kituo cha afya, miradi ambayo serikali imetoa mamilioni ya fedha na hivyo kusababisha ichelewe kukamilika.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa huyu diwani ni tatizo wala sio kwa suala la hapa shuleni, amekuwa tatizo kwa muda mrefu kwa kuwafanya wananchi kugoma kushiriki kwenye ujenzi miradi ya maendeleo na amekuwa akifanya hivyo sababu anaona hachukuliwi hatua zozote na anaona mambo yanakwenda tu," alisema.

Lwota alisema hivi karibu Mkuu wa Wilaya (DC) na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya walifika katika kata hiyo kushughulikia mgogoro wa mnada ili uweze kuhamishwa ulipokuwa kupelekwa eneo jingine lakini diwani huyo hakuzungumza chochote wala kutoa ushirikiano kwenye mkutano.

Alisema badala yake yeye na wananchi wake waliamua kuondoka kabla mkutano haujaisha.

Mkuu huyo wa wilaya aliongeza kuwa, Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Manyoni ilipofanya ziara hivi karibu katika Kata ya Mitundu, diwani huyo aligoma kushiriki.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itigi, John Mgalula, alisema kimsingi diwani wa kata ya Mitundu amekuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusababisha baadhi ichelewe kukamilika kutokana na kukosekana kwa nguvu kazi ya wananchi.

"DC ni mgeni lakini ameshaligundua tatizo lililopo kwenye kata hii, na leo Mheshimiwa RC tulikuwa timejiandaa utuchape maana utekelezaji wa miradi kwenye kata hii kasi yake sio kubwa kwa sababu ya diwani kugomesha wananchi," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Manyoni, Barnabas Mushi, alisema CCM inafahamu changamoto ya diwani huyo ambaye ana misuguano na watu wa eneo lake na chama kinaendelea kulifanyia kazi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Diwani wa kata ya Mitundu, Masanja alijitetea kuwa tuhuma hizo sio za kweli hawezi kuhamasishwa wananchi wagome kushiriki nguvu kazi na kwamba mikutano iliyofanyika ya viongozi wa wilaya wa chama na serikali hakuweza kuhudhuria kwa kuwa, alikuwa amewekwa ndani.

Serukamba alimtaka diwani huyo kubadilika na kuacha tabia hiyo ya kugomesha wananchi kwani serikali imeleta mamilioni ya fedha kwenye kata hiyo ili miradi itekelezwe na kukamilika kwa wakati kwa kushirikiana na wananchi.

## CCM yataka kasi miradi ya maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Vijijini, kimeitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) kuongeza kasi ya ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu, ili kufikisha maji safi na salama kwa wananchi wa vijijini.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Edward Ngelela, alitoa agozi hilo juzi wakati wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama hicho, walipotembelea kuona utekelezaji wa miradi ya majisafi na salama kwa wananchi wa wilaya hiyo.

Alisema wameridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo wilayani hapa lakini wanataka kasi iongezwe kukamilisha ili wananchi wa maeneo ya vijijini ambayo miradi inatekelezwa waanze kutumia maji salama na kuondokana na matumizi ya maji machafu.

"Tunataka SHUWASA mkamilishe miradi hii ya maji haraka ili wananchi waanze kupata huduma ya maji safi na salama. Kazi hii ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa vitendo," alisema Ngelela.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa SHUWASA, Sarah Emmanuel, alisema katika miradi ya maji ambayo wanaitekeleza Shinyanga vijijini, tayari baadhi wameshaanza kupata huduma hiyo wakiwamo wakazi wa Didia na Tinde na kwamba katika vijiji vingine kikiwamo cha Buchama, watafikishiwa huduma hiyo karibuni.

Nao baadhi ya wananchi wa Shinyanga Vijijini, waliipongeza serikali kwa kutoa fedha na kutekelezewa miradi ya majisafi na salama na kuomba miradi hiyo iwafikie wananchi wote na si baadhi ya maeneo.

# Wakulima 300 wapatiwa mafunzo ya elimu kilimo bora

**Na Maulid Mmbaga,** MBEYA

KAIMU Meneja wa Kampuni ya uzalishaji wa mbegu mbalimbali zikiwamo za alizeti na mahindi ya Highland Seed Growers Ltd, Elizabeth Mallya, amesema wakulima 300 wamepatiwa mafunzo juu ya kilimo bora cha alizeti na kanuni za kilimo bora kwa ujumla.

Akizungumza na Nipashe jana mkoani hapa, alisema wakulima wengi kwa sasa wamekuwa na muamko mkubwa kuingia kwenye kilimo baada ya kupatiwa elimu na kuona tija ya mbegu bora, na kwamba wanashirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT) kuhakikisha kuwa wakulima wakubwa na wadogo wanafikiwa na mbegu bora.

"Changamoto kubwa kwa wakulima walikuwa wanapata mbegu zisizo na ubora, na kusababisha kupata mavuno hafifu ila kwa sasa mbegu tuliyokuwa nayo inakubali kila mazingira hata ukipanda mbegu moja inaota na inazaa sana.

"Kwa sasa tuko katika mpango wa kuzalisha mbegu tani 100, 50 chini ya mradi na 50 zikiratibiwa na kiwanda, lengo ni kuhakikisha kwamba kila mkulima nchini anafikiwa na mbegu bora kwa ajili ya kufanya kilimo chenye tija," alisema Mallya.

Meneja Uzalishaji wa kampuni hiyo, Iddi Omari, alibainisha kuwa uzalishaji wa alizeti kwa sasa umeongezeka baada ya kuhamasisha kilimo cha kisasa na kuwapatia wakulima elimu ya kutumia mbegu bora kwa kushirikiana na AMDT na TARI chini ya mradi wa uzalishaji mbegu bora.

Alisema pamoja na uzalishaji kuongezeka lakini bado mbegu zilizopo hazitoshelezi kutokana na kiwango kikubwa cha uhitaji, ikiwa ni matokeo ya kampeni ya mradi wa uhamasishaji wa matumizi ya mbegu bora ambao umesaidia kuleta muamko mkubwa kwa wakulima.

"Wakulima wameona hizi mbegu za alizeti zilivyo bora kwahiyo wameongeza mahitaji msimu huu wanahitaji mbegu zaidi baada ya kuona uzalishaji wake ulivyo, juzi tulienda mkoa wa Rukwa wakulima walikuwa na hamu ya kutaka kujua kuwa mbegu watazipata kweli.

"Mradi umesaidia kwa kiasi kikubwa idadi ya wakulima imeongezeka, kutoka 300 ambao wananufaika moja kwa moja kwenye mradi, kuna wengine zaidi ya 1000 watanufaika kupitia mbegu tunazoendelea kuzalisha," alisema Omari.

Aliwashauri wakulima mbalimbali kutumia mbegu bora ya alizeti kwa sababu zote za msimu zimetoka katika taasisi za tafiti za hapa nchini kama TARI Ilongo, na kwamba zinaendana na kiwango cha kimataifa.

Vilevile, alisema mkulima akitumia mbegu bora zilizofanyiwa tafiti ataongeza kipato chake cha mavuno kwa ekari, akieleza kuwa wengine wanalima wakipata gunia mbili wanaridhika na kwamba kwa kutumia mbegu bora mkulima anaweza kupata hadi gunia 16 kwa ekari.

"Mbegu hizi pia hazina magonjwa yanayosababisha mavuno yashuke, ukubwa wa kichwa cha ufuta ndio unaongeza mavuno na kiuchumi itamsaidia kurudisha gharama na kupata fedha ya ziada.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suala la wazazi kujijazia kadi kliniki kamwe lisipewe nafasi

**KATIKA** gazeti la Nipashe juzi, moja ya habari zilizobeba uzito wa juu ni kuhusu kinamama wenye watoto walio katika umri wa kuhudhuria kliniki (chini ya miaka mitano), wamebainika kujijazia kadi za kliniki za watoto wao badala ya watoa huduma za afya katika vituo vinavyotoa huduma hizo.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni na watoa huduma za afya ya mama na mtoto kutoka Hospitali ya Teule ya Wilaya ya Mbeya ya Ifisi, iliyoko Mji wa Mbalizi, nje kidogo ya jiji la Mbeya. Kitendo hicho ni hatari kwa maendeleo ya afya ya mtoto hasa katika ukuaji na inaweza kuchangia udumavu kwa Watoto.

Kwa mujibu wa Ofisa Muuguzi Msaidizi wa hospitali hiyo, Herieth Mwasenga, hali hiyo ilibainika kupitia kliniki kwamba baadhi ya wazazi, badala ya kuwapeleka Watoto kliniki kama inavyoshauriwa na wataalamu wa afya, hujijazia kadi hizo kuonyesha watoto wana maendeleo mazuri kiafya.

Kutokana na kuwapo kwa vitendo hivyo, ofisa huyo aliweka bayana kwamba kuna athari kubwa kwa ukuaji na maendeleo ya mtoto kwa kuwa ni vigumu kubaini iwapo mtoto ana tatizo kiafya. Kwa kawaida, mama anapompeleka mtoto kliniki anapata fursa ya elimu kuhusu mtoto kwa maana ya afya pamoja na malezi yake yawe ya aina gani. Pia katika kliniki, wazazi wanapewa elimu kuhusu uzazi wa mpango, jambo ambalo ni muhimu kwa ustawi wa familia.

Licha ya kubainika katika hospitali hiyo, ilielezwa kuwa tatizo la kinamama kujijazia kadi za kliniki limekithiri vijijini Mbeya na kwamba baada ya kugundua hilo, elimu imeanza kutolewa kupitia utaratibu wa mara moja kwa wiki, siku ya Alhamisi ambayo pia ni maalum kwa ajili ya kutoa chanjo.

Kuwapo kwa taarifa hizo kunaibua hisia tofauti kuhusu hali ya ukuaji wa watoto hasa ikizingatiwa kuwa tatizo la udumavu kwa rika hilo linazidi kuwa kubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi. Kilichoibuliwa Mbeya ni sampuli tu ya tatizo la baadhi ya wazazi kutowapeleka watoto wao chini ya kliniki kama inavyoshauriwa na wataalamu wa afya. Baada ya kuwapo kwa habari hiyo, baadhi ya watu walibainisha kuwa jambo hilo si geni kwa kuwa liko sehemu mbalimbali na kwamba wanaohudhuria kliniki ya mama na mtoto ni wachache kulinganisha na uhalisia. Wako pia waliosema wauguzi wenyewe wamekuwa wakiwaambia kinamama wenye watoto wajaze kadi hizo wenyewe kwa kuwa wana majukumu mengi.

Ni dhahiri kwamba tatizo limeshajulikana na ni wakati mwafaka sasa serikali kupitia wizara ya afya na mamlaka za serikali za mitaa kuanzia ngazi ya kitongoji na mtaa hadi halmashauri kuchukua hatua zinazostahili. Tunasema hivyo kwa sababu katika ngazi za chini, kinamama wenye Watoto chini ya miaka mitano, wanaotakiwa kuhudhuria kliniki wanajulikana, hivyo kuwa rahisi kufanya ufuatiliaji wa karibu.

Kama ambavyo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kupitia idara ya afya imeanza kulifanyika kazi tatizo hilo kwa kuanzisha kampeni ya kila Alhamisi kufuatilia mpango wa kliniki, ni wakati mwafaka sasa kwa maeneo yote nchini kuanzisha kampeni hiyo ili kubaini wale wanaopuuza mpango huo wa afya ya mama na mtoto.


Ni wazi kwamba iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa na wazazi kuendelea kujijazi kadi, kuna hatari kubwa kwa taifa kuwa na watoto wenye udumavu na matatizo mengine ya akili. Mama anaweza kujijazia kadi kuonyesha kuwa mtoto anaendelea vizuri kiafya lakini jambo la kujiuliza ni kwamba anajuaje kama mtoto utosi wake unakomaa vizuri au hana ukosefu wa damu na matatizo mengine ya kiafya?

Wahenga wanasema msingi mzuri wa maendeleo ni mwanzo wa jambo, hivyo hata maendeleo ya watoto kimakuzi na kiafya yanategemea sana ukuaji wao tangu wakiwa na umri chini ya miaka mitano. Katika umri huo, watoto wanajengewa msingi bora kiafya na ukuaji huku suala la kliniki likipewa kipaumbele.

Pia ikumbukwe kwamba watoto ni taifa la kesho na hakuna taifa linaloweza kuwa na maendeleo bila watu wake kuwa na afya, hivyo suala la afya bora kwa Watoto si la kufanyiwa mizaha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Programu hii ilete matokeo chanya ya malezi



Na Sabato Kasika

**SERIKALI** imeanzisha programu ya mafunzo ya Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto yenye lengo la kuimarisha malezi ambayo yatasaidia kuwa na jamii bora.

Kupitia utekelezaji wa programu hiyo jumuishi ya taifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto iliyozinduliwa Desemba mwaka, 2021, ili kutekeleza na kuleta matokeo chanya kwa taifa.

Programu hiyo inayohusu umri mwaka sifuri hadi nane, inashirikisha watu wa kada mbalimbali, wakiwamo maofisa ustawi na maendeleo ya jamii na wadau wengine kutoka asasi za kiraia.

Ninaamini kwamba elimu hiyo kwa kada hizo ni mwanzo wa kuzifikia kada nyingine na inaweza kukuza uelewa na kusaidia kusimamia maadili mema ambayo yameporomoka katika jamii.

Mmomonyoko wa maadili umekuwa ukitajwa kuwa chanzo cha kuwapo kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto, hivyo kuibuliwa kwa programu hiyo kuwe ni chachu ya kuibadili jamii.

Suala la malezi na makuzi mazuri kwa watoto linagusa pia lishe bora kwa afya zao, ambapo wazazi, walezi na jamii wanatakiwa kuelimishwa, ili watambue umuhimu huo na kuutekeleza kwa vitendo.

Kwa ujumla ni kwamba programu hiyo ni kielelezo tosha cha jinsi ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan ameamua kujielekeza katika kuweka misingi imara ya malezi na makuzi ya watoto wa taifa hili.

Hatua hiyo inaweza kusaidia kuwa ni fursa ya kukuza vipaji vya watoto tangu hatua za awali za ukuaji wao na hivyo kufika mbali katika kutoa machango wao kwa taifa lao.

Kwa kuwa serikali inatambua mafunzo hayo na fursa zake za kulijengea uwezo kundi kubwa la wataalamu watakaokuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu utekelezaji wa programu, ni vyema jamii iwe tayari kuelimishwa.

> **Kwa kuwa serikali inatambua mafunzo hayo na fursa zake za kulijengea uwezo kundi kubwa la wataalamu watakaokuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu utekelezaji wa programu, ni vyema jamii iwe tayari kuelimishwa.**

Ni wazi nchi itakuwa na wataalamu wengi kwenye maeneo mbalimbali na kuwa na uhakika kuwa programu hiyo inaratibiwa na kusimawiwa na watu sahihi wenye uelewa katika malezi na makuzi ya watoto.

Elimu kwa kada hizo ni mwanzo wa kuzifikia kada nyingine, ili ziweze kuwa karibu na kuhakikisha jamii inakuwa na uelewe wa namna ya kuwapa watoto malezi bora kupitia programu hiyo.

Ninadhani matarajio ya wapenda malezi bora ni kuona maofisa ustawi na maendeleo ya jamii, kuwa na kazi ya kwenda katika vituo vyao vya kazi nchi nzima ya kuweka mipango ya kuifikia jamii na kuipa elimu hiyo.

Kumekuwapo na vitendo vya ukatili kwa watoto, huku chanzo chake kikiwa ni malezi duni, na sasa ni vyema kufichua viashiria vya vitendo hivyo vinavyotokea nyumbani na hata shuleni.

Takwimu ambazo zimewahi kutolewa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Makundi Maalum, ni kwamba matukio ya ukatili kwa watoto katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka 2019, yaliyoripotiwa ndani ya Jeshi la Polisi ni 11,499 ikilinganishwa na matukio 15,870 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na upungufu wa imatukio 4,371 ikiwa na asilimia 27.5

Mikoa iliyoongoza ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500), Mkoa wa Kipolisi Ilala (489), makosa mengi yakiwa ni ubakaji (5,899), mimba za wanafunzi (1,677) na ulawiti (1,114).

Hivyo, kupitia programu hiyo, ni wazi kwamba iwapo waliopata mafunzo watatimiza wajibu wao inavyotakiwa, inaweza kuleta ilete matokeo chanya katika malezi bora.

## FIKRA MBADALA

# Hakuna ubaya wowote kusaidiwa unaposhindwa



Pascal Mayalla

MAKALA ya leo ni wito kwa Watanzania wenzangu, tujifunze kujikubali kuwa hatuwezi kila kitu. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo inaweza kila kitu yenyewe, hivyo hakuna ubaya wowote kwa mtu yeyote, taasisi yoyote, au nchi yoyote kusaidiwa pale inaposhindwa.

Kuna vitu Watanzania wenyewe hatuwezi na inapotokea hivyo, tunapojaribu kuvifanya na tukashindwa, lazima tukubali kuwa tumeshindwa, hatuwezi. Swali ni je, unaposhindwa kuna ubaya wowote kukubali kusaidiwa au kuendelea kujitutumua mpaka uweze huku mambo yakiharibika?

Ni dhahiri kabisa mpango wa kutaka kuipa kampuni ya Dubai kuendesha bandari ya Dar es Salaam, ni uamuzi sahihi, tena kwa maoni yangu, si bandari pekee. Hata kuendesha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwa faida sisi wenyewe hatuwezi, lazima tuingie ubia. Hata tukija kwenye reli ya kisasa (SGR) tunayoijenga ndiyo kabisa. Bila kuuma maneno lazima tushirikiane na wajuvi wenye uzoefu, wakati tukijenga uwezo wetu wa ndani.

Kuna vitu Watanzania hatuwezi na tunashindwa si kwa sababu hatuna akili au hatuna uwezo bali kwa sababu tu hatujui kutazama mbali. Mfano hivi sasa tumepamba moto kujenga SGR lakini hatuna mkakati wowote wa kujiandaa kwa mzigo wa kuiendesha kwa faida.

Kuendesha SGR kwa faida si mchezo. Wenzetu Kenya yameshawakuta, wanaiendesha SGR yao kwa hasara. Je, sisi tusubirie SGR yetu ikamilike, tujaribu kuiendesha tushindwe ndipo tutafute usaidizi? Au wakati ujenzi unaendelea, tutazame mbali kwa kujenga uwezo wa uendeshaji na maandalizi ya kutafuta mzigo wa kushiba wa kubebwa na SGR.

Hivi sasa tuna reli ya TAZARA, inayotoka Dar es Salaam mpaka Kapiri Mposhi nchini Zambia, tumeshindwa kuiendesha, Tunduma ni eneo lililochangamka kibiashara na mizigo ya Zambia inabebwa na malori huku mabehewa ya TAZARA yakiwa yamelala bure.

Reli ya kati ambayo ni kongwe inayoanzia Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma pamoja na kipande cha Kaliua hadi Mpanda na pia kutoka Dar es Salaam hadi mikoa ya kaskazini tumeshindwa kuiendesha. Nenda bandari kavu ya Isaka, ukiwa mzalendo mwenye machozi ya karibu, unaweza kulia. Mtu aliyeshindwa kuendesha kidogo hiki uje umpe kukuendeshea SGR, unategemea nini? Kuna ubaya kuwaita watu wenye uwezo wakuendeshee kwa kipindi fulani huku ukijenga uwezo wa ndani na ukiwa tayari ndipo uendeshe?

ATCL, tumshukuru Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli, Mungu amrehemu, kwa kuchukua uamuzi mgumu wa kukimbilia kununua ndege kwa fedha taslimu. Lakini kosa la kiufundi lililofanyika ni kununua ndege bila kuwa na mpango biashara ili kuleta tija kwa shirika.

Tumenunua ndege za masafa marefu lakini zinafanya safari Dar es Salaam - Mqwanza na KIA. Matokeo yake kwa sasa ndege nne hazifanyi kazi kwa uchovu wa injini. Hii SGR tutatengeneza kwa kwa mabilioni ya dola halafu tuje kuharibu tena! Ukiangalia abiria wa Tanzania wanaokwenda Ulaya na America kwa ndege za mashirika mengine ni abiria wa kujaza ndege za siku saba lakini sisi wenyewe hatuzitumii ndege zetu kiufanisi. Hatuwezi ni lazima tusaidiwe.

Pale unaposhindwa kitu fulani, hakuna ubaya wowote kuomba msaada kwa wenye uwezo usaidiwe. Tuliwahi kujaribu kwa ATCL, Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL- sasa Shirika la Mawasiliano Tanzania), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mamlaka ya Majisafi na Usafiri wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa kuanzisha City Water, tukaja kuvunja mikataba hiyo.

Kuna msemo wa Kiswahili usemao "Ukitaka kula ni lazima uliwe!", hivyo hata katika suala hili la bandari, kwa vile tunataka kula, ni lazima tuliwe. Kuna vitu vingi tunashindwa na tunaomba msaada tunasaidiwa. Jengo la Benki Kuu ya Tanzania (BoT) lilipoungua, polisi wetu walishindwa kufanya uchunguzi, tuliomba msaada wa polisi wa Uingereza, The Scotland Yard, wakatusaidia.

Miaka kadhaa iliyopita, aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, alishambuliwa kwa kupigwa risasi mchana kweupe. Ben Saanane wa Jamii Forums na Azory Gwanda wamepotea katika mazingira ya kutatanisha na hakuna uchunguzi uliofanyika. Miaka inakwenda bago giza nene juu ya watu hawa!

Kiukweli ni kwamba serikali yetu imeshindwa kufanya uchunguzi wa matukio hayo kwa sababu hatuna uwezo huo lakini tumeona aibu kuomba msaada ili tusaidiwe. Matokeo yake watu wasiojulikana bado wapo wanajivinjari tu.

Kuna watu wanadhani Scotland Yard, wanazaliwa na uwezo huo! Hapana, wanafanya 'scouting' kuwapata watu wenye uwezo huo. Hata hapa Tanzania tunao watu wa namna hiyo lakini hatuwatumii.

Niliwahi kuuliza Wana Jamii Forums je, tuisaidie serikali yetu inaposhindwa au tusubiri ishindwe, tuibeze na kuizomea kuwa haiwezi?

Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere japo alitupatia uhuru, kulikuwa na watu wengine wenye uwezo kuliko yeye, wangeweza kututawala vizuri zaidi na kutufikisha mbali Zaidi lakini ndiye aliyechaguliwa na Mungu kuwa Rais wetu. Vivyo hivyo, kwa Ali Hassan Mwinyi, Banjamin Mkapa, Jakaya Kikwete, Magufuli na sasa Samia Suluhu Hassan, haina maana kuwa ndio wazuriv kuliko Watanzania wote lakini ndio waliochaguliwa. Lakini ukweli ni kwamba wako watu wazuri na tunaweza kuwaita 'vichwa' wamejinyamazia tun a wanaangalia kwa sababu hawajaombwa wala kushirikishwa.

Wito kwa serikali yetu tukufu, tukishindwa jambo lolote, kabla hatujakimbilia huko nje kuomba msaada, tuangalie uwezo wetu wa ndani. Tuwaulize au kuwatafuta kwanza Watanzania wenye uwezo wa kusaidia.

Serikali ijitokeze kwa uwazi kabisa na iseme wazi kabisa kuwa hili limetushinda, kama kuna Mtanzania au kampuni ya Kitanzania inaweza kusaidia na ina uwezo huo, ijitokeze. Ikitokea hakuna Mtanzania au kampuni ya Kitanzania yenye uwezo huo, ndipo tutafute wabia kwa kutangaza kwa uwazi kabisa, mabingwa wa uendeshaji wa bandari duniani washindane kwa ushindani wa wazi na tumpe mshindi.

**Paskali**
**0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tusiumize watoto kiakili tuache wapumzike



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

NI kawaida wazazi wanapoozesha watoto wao, huwa na shauku ya kupata matokeo haraka kutokana na ndoa iliyofungwa, nayo ni kupata watoto wakitamba ndoa imejibu.

Familia hiyo mpya ya wanandoa wapya inapochelewa kuleta matokeo, minong'ono huanza na hata inapotoa matokeo ya haraka haraka na tena kwa mfululizo, utasikia, hivi hampumziki!

Ni sawa kabisa na familia inapokuwa mathalan na gari moja na kila mmoja anataka alitumie, huyu akiliendesha akirudi huyu analichukua, utasikia jamani hilo gari halipumzishwi?

Hata katika maisha ya ufanyaji kazi, ndiyo sababu katika jamii yoyote kuna siku za mapumziko hususan mwishoni mwa wiki, wakiiga siku ile tunayoambiwa ya saba ambayo Mungu alipumzika.

Pia michezoni, watu wanacheza, lakini kuna muda utasikia sasa ni wakati wa mapumziko. Watu wanakaa na kujipoza miili na kisha kurudi kuendelea na mchezo au mashindano.

Mifano hii michache inaonYesha umuhimu wa mapumziko katika karibu kila fani ya maisha ya binadamu. Hata wanyama nao hupumzika huko waliko kwa kutegemea shughuli zao.

Hivi sasa nchini kumezuka mjadala mzito, unaohusu mapumziko ya wanafunzi shuleni na hata vyuoni, lakini hasa shuleni kuliko na wanafunzi ambao bado wanategemea wazazi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, anapambana sana na hili la mapumziko kwa wanafunzi na kwa kiasi fulani amefanikiwa licha ya vizingiti vya hapa na pale.

Ni dhahiri kuwa akili ni kiungo muhimu sana katika mwili wa binadamu na kinashirikiana kwa karibu sana na moyo kuhakikisha kuwa maisha ni timamu, hivyo akili imekuwa ikifanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha uhai unakuwapo na hivyo kuhitaji pia kupumzika, ili kujijenga upya kwa mapambano mengine.

Akili inapokosa kupumzika, ndipo unaposikia uchovu uliokithiri, hivyo kuhitaji usingizi ili kujipanga upya. Kinyume cha hapo, ndipo unaposikia huyu kachanganyikiwa na kuwa kichaa.

Ndiyo sababu pia mtu akosapo usingizi mfululizo kwa muda mrefu, huhatarisha maisha yake na inawezekana hata yakapotea kwa jambo hilo linaloonekana dogo.

Watu wazima wanajua ni nini maana ya uchovu wa kiakili na ni nini umuhimu wa mtu kupumzika anapokuwa ameshafanya kazi nyingi kwa kutumia nguvu ya akili na mwili.

Lakini inashangaza ni hao hao watu wazima wanaojisahaulisha kwa sababu wazijuazo wao, na kutaka watoto wao wafanye kazi kubwa ya kiakili bila kupumzika.

Wanataka mtoto asome mfululizo na hata nyakati za mapumziko ambazo zimepangwa, hivyo hubuni njia nyingine eti za masomo ya ziada au kambi, ili mwanafunzi huyo endelee kusoma.

Hawataki mtoto aende likizo, wakiamini kwamba kubaki kwake shuleni kwa mlango mwingine, ndiko kufanikiwa darasa la nne, darasa la saba, kidato cha pili na cha nne!

Inashangaza hata baadhi ya wamiliki wa shule wanalijua hili fika na wengine tena wakiwa wawakilishi wa wananchi, kuunga mkono kadhia hii ya kulazimisha watoto kubaki shuleni nyakati za likizo.

Wakiulizwa, wanaharakisha kujibu eti wazazi ndio wamekubaliana! Hawajui wazazi hao ni wale wapenda sifa wasiohurumia watoto wao kiakili, ili mradi wanataka eti wafaulu.

Lakini wamiliki wa shule nao wanajua wanachokifanya, kwamba wanawakamua wazazi hao fedha za ziada mbali na ada, na kujipatia mapato zaidi ya bila kodi, kutokana na biashara hiyo.

Mtoto akipumzika baada ya muhula wa masomo, akiwa nyumbani hubadili hali ya hewa kiakili, anakutana na mambo asiyoyaona shuleni na hivyo akili kutulia kwa kuona mapya.

Mathalan, mtoto kuna somo analichukia, kuna mwalimu anamchukia, kuna mazingira anayachukia, hivyo anapokuwa likizo, anakuwa mbali na mambo hayo, hivyo akili kutulia kwa muda.

Tufike mahali tuache kutania akili za binadamu, tuhurumie watoto wetu kwa kupitisha sheria zinazowalinda dhidi ya kadhia hizi, ili likizo iwe kweli likizo na watu wapumzike. Na itawezekana iwapo walimu watasimamiwa wafundishe vizuri kwa wakati na ukamilifu.

Kubembelezana kukiendekezwa katika afya za binadamu, tutakuja kulia na kusaga meno baadaye, kwa kulea kizazi chenye maumivu kwa sababu ya tamaa za wafanyabiashara na sifa za wazazi wasioona mbali.

Mapumziko ni dawa ya akili na mwili, mapumziko ni dawa ya roho na moyo, kuyabeza ni kubeza maisha. Tumsikilize Waziri Mkenda, tumsaidie kuendesha Wizara yake kwa maslahi mapana ya taifa la leo na kesho.

**Alamsiki!**

# Wanandoa vikongwe walilia fidia nyumba yao kubomolewa

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa** NANYUMBU



Mzee Laisa Mmole (98) na Mkewe Bibi Sigele Mtehiya (91) wakiwa katika makazi yao.

NI hofu, huzuni, giza nene mbele yao huku kwa umri wao wanapaswa kuhurumiwa. Hiyo ndiyo picha halisi kwa vikongwe Laisa Mmole mwenye umri wa miaka 98 na mkewe, Sigele Mtehiya (91) kutokana na maisha wanayoishi hivi sasa yakiwa hayana matumaini hata kwa kesho.

Wazee hao wanaishi maisha ya taabu baada ya kulazimika kuhama nyumba yao na kwenda kijijini kutokana na kupisha ujenzi wa barabara.

Kutokana na Maisha wanayoishi, wanaiomba serikali kuwasaidia kwa kuwalipa fidia ya fedha kutokana na nyumba yao kuwa ndani ya hifadhi ya barabara ya Mangaka hadi Mtambaswala inayounganisha Tanzania na Msumbiji.

Vikongwe hao wanasema wamelazimika kuihama nyumba hiyo iliyoko katika kijiji cha Namasogo, Kata ya Chipuputa, Nanyumbu mkoani Mtwara, baada ya watalaamu kuweka alama katikati ya nyumba kuonyesha ukubwa wa barabara hiyo. Kwa maana hiyo, nyumba hiyo iko kwenye hifadhi ya barabara, hivyo wanapaswa kuondoka na wakafaya hivyo.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hii, aliyetembelea kijijini hapo na baadaye shambani wanakoishi hivi kwa sasa, vikongwe hao wamesema alama hiyo iliwekwa tangu barabara hiyo ujenzi wake ukiendelea hadi ilipokamilika miaka miatatu iliyopita.

Wanasema hata kama nyumba yao haikuwekwa katika mpango wa kufidiwa, wanaiomba serikali kuwaangalia kwa jicho la ziada na huruma na kuwalipa kwa sababu hawawezi tena kuitumia.

"Kama ulivyoiona, nyumba imeanza kubomoka na hatuwezi tena kuishi ndani yake. Tunaiomba serikali itusaidie kutulipa ili tujenge nyingine katika maeneo yanayostahili," anasema Bibi Sigele.

Mzee Mmole anasema serikali ndiyo kila kitu na ina uwezo wa kuwafidia si tu kwa sababu wao ni wazee, bali nyumba yao iko sambamba na nyumba za majirani ambao wote wamefidiwa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Namasogo, Jafari Visa, anasema wazee hao waliwasilisha malalamiko yao ofisi za kijiji na kuongeza kuwa mwishoni mwa Mei, mwaka huu, aliitwa ofisini kwa Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu kuzungumzia jambo hilo.



Bibi Sigele (91)

"Ni kweli wazee Mmole na mkewe Sigele wamewahi kuwasilisha malalamiko yao wakihoji kwa nini wasilipwe fidia ya nyumba yao kama ambavyo serikali imefanya wa wakazi wengine hasa majirani zao," amesema.

Mwandishi aliwasiliana na Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Mtwara, Mhandisi Dotto John, ambaye alijibu kwamba mradi wa ujenzi wa barabara hiyo ni wa kitaifa, hivyo si vibaya wakaulizwa viongozi wa ngazi ya kitaifa.

Hata hivyo, mtoto wa vikongwe hao, Stambuli Mmole, aliwahi kuwasilisha barua ya malalamiko ofisi za TANROADS Mkoa wa Mtwara, lakini akaambiwa majibu yalishatumwa kupitia masjala ya Mkuu wa Wilaya.

Baada ya kuambuwa hivyo, anasema alifika ofisini hapo mara kadhaa, lakini akaambiwa kwamba barua hiyo haijaonekana.

Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, Mariam Chaurembo, alithibitisha kuwapo kwa jambo hilo na kwamba alimwita Mwenyekiti Jafari katika kikao cha pamoja kati yao, maofisa wa serikali ngazi ya wilaya, viongozi wa TANROAD Mkoa na ujumbe maalum kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Kikao kilifanyika ofisini kwangu na baada ya majadiliano, tukaona kuna umuhimu wa kwenda hadi kijijini Namasogo.

Wataalam kutoka ofisi za TANROADS Mtwara walipima kutoka barabarani hadi nyumba hiyo ilipo na kuonyesha iko ndani ya mita 22," anasema.

DC Chaurembo anasema wahisani waliojenga barabara hiyo, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), walilipa fidia watu wenye nyumba au mazao yaliyoonyesha tu kama yangeendelea kuwepo yangekwamisha maendeleo ya mradi.

Hata hivyo, Chaurembo anasema baada ya ziara hiyo, ofisi yake imetoa mapendekezo na ushauri kwa Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya hatua za kuchukua ili kushughulikia jambo hilo ambalo ni la muda mrefu.

Mwanzoni mwa sakata hilo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Nanyumbu, Salum Palango, alipoulizwa kama anatambua kuwapo kwa malalamiko ya vikongwe hao, alisema: "Nakushauri wasiliana na ofisi ya TANROADS Mkoa wa Mtwara ambako ndiko kuna majibu stahiki ya kisheria."

Afisa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Andrew Makota, anakiri jambo hilo limefika ofisini kwao na tayari wamewasiliana na ofisi ya Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mtwara ili kupata maelezo ya kina juu ya malalamiko ya wananchi wa kijiji hicho, hasa vikongwe hao.

"Tunalo jukumu la kufuatilia ili tujue nini kimetokea. Tunaamini baada ya muda mfupi ujao tutapata majibu ya kudumu," alisema Makota akiwa jijini Dodoma.

Wakati hayo yakiendelea, zimepita siku zaidi ya 530 sasa tangu vikongwe hao wahame kwa lazima kijijini hapo na kwenda kuishi shambani baada ya nyumba yao kuanza kubomoka.

Mara kadhaa, vikongwe hao kupitia mitandao ya kijamii wamesikika wakipaza sauti zao wakiomba Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuwasaidia walipwe fidia ya nyumba yao kabla hawajafa.

Mbali na vikongwe hao, wananchi wengine wanaolalakamikia kutolipwa fidia zao ni pamoja Eleza Omari na Jafari Machomela. Ingawa wamekiri wanachodai sasa ni mali chache zilizokuwa zimesahaulika, tofauti na ilivyo kwa Mzee Mmole na Bibi Sigele ambao hawajalipwa kabisa.

**Angalia picha cha vikongwe hao na makazi yao mapya shambani baada ya nyumba yao iliyopo Namasogo kijijini kuanza kubomoka.**



Mzee Mmole (98)

# MAISHA

JUNI 11, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14


## JILAMBE NA SUPU YA PWEZA

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Fanya uchaguzi sahihi wa sakafu ya nyumba




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# Maji, chumvi yanavyoweza kungarisha uso wako

Ukurasa 14


**MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA**





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | M | A | M | B | A |
| S | | | | W | | S |
| I | | L | I | A | | H |
| K | O | A | | K | A | U |
| I | | A | N | A | | S |
| T | | N | | | | H |
| I | Z | A | M | E | | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


NIA, BEE, MIE, BAO, PANDE, AMANA, NEEMA, BONDA, PAMBANA, ENDELEA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

HERUFI HIZI ZILIZOVURUGWA ZINABEBA MAJINA YA MIKOA MIWILI, HEBU ZIPANGE!




## WATOTO

# PAKA RANGI



@ A.MSAMBA

CHEKA

KICHEKESHO

BAADA YA JAMBAZI KUVAMIA KANISA

Jambazi mmoja aliingia kanisani na bunduki akapiga risasi juu ya bati akasema “asiyempenda YESU atoke nje” wakatoka wote isipokuwa mchungaji na wazee wawili.

Jambazi likamwambia mchungaji “unaweza kuendelea na ibada, nilikuwa nakuondolea wanafiki”, Mchungaji akasema “ungewaacha kwanza nichukue sadaka...!

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mambo mke anapaswa kufahamu kuhusu wakwe

KARIBU msomaji wangu tuendelee kuelimishana kuhusu mambo mbalimbali yanayotusibu kwenye maisha yetu na namna ya kuyatatua. Iko misingi na kanuni ambazo tunapaswa kuzingatia ili maisha yawe mazuri na tulivu.

Ndoa nyingi zinapata misukosuko mingi kwa sababu tu wanandoa wenyewe wanakiuka misingi bora ya maisha. Nikuambie leo msomaji wangu, ndoa si tu kuvalishana pete kama tamko la agano au mkataba wa maisha unavyotafsiri.

Wanawake wengi leo wako katika sintofahamu nyingi kuhusu ndoa zao. Wengine wamezikimbia, wengine wamejitia nguvu kutegemeana na yale wanayopitia. Wengine wamepoteza maisha kwa sababu tu hawakuzingatia mambo ya msingi.

Leo nimkazie macho mke. Kama unatamani kuishi maisha marefu na kuwa na amani kwenye ndoa yako, yapo mambo unapaswa kufahamu. Ni maelekezo unayohitaji ili kuwa na faida ya kudumu. Usiyapuuzie yanaweza kubadili kabisa sura ya nyumba yako na ndoa yako!

Kwanza, elewa kuwa mume wako ni mwanaume na yuko tofauti na wewe. Pia tambua vipo vitu anataka uvijue. Mume wako anataka umtii, umheshimu, umpende na kumpa kipaumbele. Mwanaume anataka umpende kutoka moyoni.

Anataka upende vitu anavyovipenda akiwa hayuko kazini. Anataka na wewe ulete mchango wako katika kujenga uchumi wa familia. Anataka uwe mwaminifu na kutunza siri zake.

Anataka watoto wawe wasafi wakati wote na anataka kula chakula kizuri. Anataka awe mtu wa kwanza katika maisha yako, kama mama yako alivyo mtu wa kwanza katika maisha yako! Naye (mume) atamfanya mama yako mzazi kuwa mtu wa kwanza kwenye maisha yake.

Pili, tambua kuwa mume wako ana wazazi wake. Wanawake wengi wanapoingia kwenye ndoa, hupuuzia sana eneo hili ndio maana wanapata madhara makubwa katika maisha. (mifano hai ipo tutajadili wiki ijayo).

Wake wengi huwa wanaishi kana kwamba waume zao walitoka mbinguni na kwamba hawana wazazi, huku wao wakiwahudumia wazazi wao. Hii ni hatari sana! Kama utashindwa kutambua kuwa mume wako ana wazazi, na kwa mantiki hiyo wazazi wa mwanaume ni lazima tu watakushughulikia. Wanaweza kufikia hatua ya kukutoa kwenye nyumba ya mtoto wao!

Kingine, tambua kuwa mume wako anawapenda wazazi wake. Kosa kubwa ambalo utalifanya katika maisha yako ni kufikiri kuwa mume wako hawapendi wazazi wake. Nikuambie kuwa anawapenda sana! Nawe uwe na hekima ya kuwapenda.

Kumbuka mama mkwe ndiye aliyekuwa mpenzi wa kwanza wa mume wako. Ni mwanamke wa kwanza aliyewahi kumpenda katika maisha yake. Na bado anampenda hata kama wewe umekuwa sehemu ya maisha yake. Yakupasa kuwapenda wazazi wake bila kubagua.

Kingine, fahamu ya kuwa mume wako anataka uwapende wazazi wake. Hata kama wazazi hawa wamekufanyia ubaya wa aina gani, mume wako anatarajia uendelee kuwapenda, sawa na vile unavyowapenda wazazi wako. Ikiwa hutafanya hivyo, naye ataanza kuwachukia wazazi wako, na kuanza kukusema vibaya mbele ya wazazi wake. Ikifikia hatua hiyo, matatizo mengi yanaweza kuibuka pasipo sababu.

Mume wako anataka uwaheshimu wazazi wake. Elewa kuwa wazazi wake walimhudumia kwa zaidi ya miaka 25 kabla haujakutana naye. Hivyo, wanahitaji kupongezwa, kuheshimiwa kwa sababu, kama wasingemzaa usingepata nafasi ya kuolewa naye. Usithubutu kuua kuku aliyetaga dhahabu!

Mama mkwe hana cha kupoteza. Endapo utamvamia mama mkwe na kumdhalilisha kwa sababu yoyote ile, hutaweza kushinda vita hiyo hakika. Kumbuka kwamba mama mkwe bado ana nguvu kwa mtoto wake.

Jitahidi usimkabili kwa ukali. Mtafute kwa upole kama unahitaji maelekezo kutoka kwake na siyo kumwendea na kumjibu kwa ukali. Kama utatumia hekima utashinda, usipofanya hivyo utalaumiwa.

Kingine tambua kuwa wewe ni mrithi wa mume wako. Wifi, shemeji zako, marafiki zake, wazazi wake na kadhalika siyo warithi wake bali wewe ndiye mrithi wa mumeo. Kama bado hajakuandika mrithi wa mali zake, kaa naye na kujadili suala hili kwa hekima na kwa maombi na kuangalia uwezekano wa kubadili kwenye hizo nyaraka kama hazionyeshi wewe ni mrithi.

Pia fahamu wakwe zako wanakuchunguza, wanakufuatilia. Fahamu pia ipo siku utakuwa mama mkwe. **Wiki ijayo nitatoa mifano hai kuthibitisha yaliyowapata waliodharau wakwe. Una kisa? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Uhalifu wa kifedha, tumeamka tumechelewa

Moja ya mambo yanayoisumbua dunia kwa sasa, Tanzania ikiwamo, ni suala la uhalifu wa kifedha unaovuka mipaka.

Uhalifu wa kifedha, kama usipokuwa na makachero wabobezi kwenye tasnia ya fedha, au kitengo maalum cha FIU (Fraud Inteligence Unit), itakusumbua kupambana na makosa ya uhalifu wa kifedha, kwa kuzingatia athari ambazo hutokea kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mpaka sasa sina hakika, kama kuna nguvu ambayo tumeiweka katika mapambano haya, lakini kuna haja kwa wadau wa haki jinai, kuunganisha juhudi na nguvu kitaifa ili kupambana kikamilifu na uhalifu wa kifedha.

Utakatishaji fedha, wizi wa fedha kwa njia ya mtandao ni makosa makubwa yanayohusisha makundi ya wahalifu waliojipanga.

Hakuna nchi ambayo haijaguswa na uhalifu huu, ambao unaathiri usalama wa taifa, ongezeko lisiloelezeka la mahitaji ya bidhaa na huduma.

Uchunguzi wa kifedha na ulaghai, unaweza kusaidia kufichua uhalifu na kesi kubwa na ngumu za ulaghai, ambazo timu za makachero na wanasheria wa nyumbani wanahitaji usaidizi.

Ni kwa sababu hiyo, wanaweza pia kutambua ni nani anayehusika na kuhesabu uharibifu wowote.

Swali la kujiuliza ni je, uchunguzi wa fedha na ulaghai hufanyaje kazi? Uchunguzi wa ulaghai ni kubaini ni nani aliyehusika na ulaghai huo, nia zao zilikuwa nini, na ni kiasi gani cha pesa kilipotea katika biashara nzima?

Uhalifu wa kifedha ni shughuli yoyote ya uhalifu ambayo inahusisha kuchukua pesa au mali, ambayo ni ya mtu mwingine ili kupata faida ya kifedha au kitaaluma.

Kutokana na asili yake, athari za uhalifu wa kifedha huonekana duniani kote, kwa viwango tofauti vya ukubwa, kulingana na nguvu ya uchumi wa mataifa binafsi.

Kwenye hili kuna jambo la kujifunza kwa sababu ili kuendana na matakwa ya sheria za kimataifa, Tanzania ilitunga sheria ya utakatishaji fedha mwaka 2006.

Sheria hiyo imebainisha makosa mbalimbali ya utakatishaji wa fedha, ikiwemo mtu yeyote atakaye jihusisha moja kwa moja au kwa njia nyingine katika muamala unaohusisha mali itokanayo na mapato ya fedha haramu.

Usisahau mtu yeyote atakaye badili, hamisha, safirisha, pitisha mali akiwa anafahamu kuwa mali hiyo ni ya mapato au zao litokanalo na uhalifu, ameangukia kwenye uhalifu huu.

Aidha, kuficha, kupoteza ukweli au chanzo halisi cha mali hiyo kuwa ni haramu, utakuwa umeangukia kwenye uhalifu huu. Kwamba, mtu yeyote atakayeficha, funika ukweli, zuia upatikanaji wa ukweli, chanzo, mahali, uhamishaji wa umiliki, mzunguko, au umiliki wa au haki kuhusiana na mali hiyo, akiwa anafahamu au anapaswa kufahamu au alipaswa kufahamu kuwa, mali hiyo imepatikana kwa mapato yatokanayo na fedha haramu, ni uhalifu wa kifedha.

Binafsi, naona kama taifa hivi sasa tunahitaji kuwa na makachero wanaoweza kuja na matokeo chanya, wakiwa na uwezo wa kukusanya taarifa na kuja na ripoti ya kina.

Wakati nawaza haya, nimefarijika sana kuona Jeshi letu la Polisi limeshtukia aina hii ya uhalifu na kutafuta mbinu na mawazo mbadala ya kukabiliana nalo.

Nimemsikia Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camilius Wambura, akieleza namna walivyoingia makubaliano na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), kufundisha makachero wake kozi za Sayansi ya Polisi, mafunzo ya kimkakati, usalama wa mtandao na mafunzo ya amani na usalama. Hapa sasa ndiko kama taifa tunataka mtufikishe kule tunakotaka.

Kwamba, wazalishe wabobezi wenye taaluma ngazi ya shahada ya sayansi katika usalama wa mtandao, katika usalama na masomo ya kimkakati, na shahada ya uzamili katika amani na usalama na usalama wa taarifa.

Achilia mbali uhalifu wa kifedha unaovuka mipaka, kuna uhalifu mwine hatari ambao ni uhalifu wa mtandao. Uhalifu wa kifedha, tumeamka tumechelewa

Ni uhalifu ambao sasa unaanza kuibuka kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia duniani.


Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. **Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI





Ili kuwa shangwe na nderemo kwa Bwana James Soka na Bi.Julieth Julius, walipofunga ndoa takatifu Mei 7, katika Kanisa la Katoliki Makoka Parokia ya Mtakatifu Gaudence, baadaye kufuatiwa na tafrija fupi katika ukumbi wa Blessing Hall Tabata Segerea.





# MITINDO
Na Mary Geofrey



# Kiafrika zaidi na swaga ya kitenge


KWA namna yeyote kijana wa kiafrika wa leo lazima awe na swaga za kizalendo ambazo ni za kiafrika ikiwamo kitenge.

Kitenge wakati tunakua tulikuwa tunajua ni nguo za kuvaa watu wazima nikimaanisha wenye watoto lakini kwa sasa, vijana ndio wanaongoza kupenda kuvaa vitenge.


Kuna mishono na mitindo mbalimbali ya vitenge ambayo haikutoi nje ya fashion na kuendelea kutokelezea kisasa zaidi.

Nguo za kitenge ambazo vijana wengi wanavaa ni kutupia swaga kama shati, blauzi na gauni au kushonea kwenye pochi.

Kama ambavyo unajionea kwenye picha hizo.







URIMBO

UREMBO

## Na Mary Geofrey

# Maji, chumvi yanavyoweza kung'arisha uso wako



JINSI ya kuondoa chunusi na jinsi ya kufanya sura ionekane nzuri na ya kuteleza, bila kutumia mafuta yenye kemikali.

Leo katika safu yetu hii ya urembo tutaelekezana kwa kina njia mbili zitakazosaidia kusafisha uso wako na kuonekana mrembo.

Kunawa kabla ya kulala na baada ya kuamka

Kabla ya kulala unatakiwa kunawa uso wako na maji ya uvuguvugu, safi na salama na kufanya tena hivyo baada ya kuamka.

Siyo lazima sana kutumia maji ya uvuguvugu, unaweza kutumia hata ya baridi kwa sababu maeneo mengine unaweza kukosa huduma hiyo.

Osha kwa sabuni ambazo hazina mafuta kama jamaa au mbuni ingawa kuna zingine zina mafuta siku hizi hivyo kuwa mwangalifu.

**Safisha uso kwa chumvi**

Safisha uso na chumvi kunasaidia kuondoa seli za ngozi zilizokufa, angalau kwa wiki mara moja pale unapoona ngozi yako ina matatizo lakini pale unapoona imeanza kuleta mabadiliko unaweza fanya hata kwa mwezi mara moja.

Kutumia njia hizi mbili hazikuzuii kuendelea kutumia mafuta au losheni yako unayozoea. Utaona mabadiliko makubwa lakini ukiona umemaliza wiki mbili bila mabadiliko yoyote unatakiwa kwenda hospitali kumuona daktari.





MAPISHI

## Na Mary Geofrey

# Jilambe na supu ya Pweza nyumbani

SUPU ya Pweza imekuwa maarufu baada ya kuanza kuuzwa barabarani katika maeneo ya vijiwe na mikusanyiko mikubwa ya watu kama sokoni na vituo vya mabasi na daladala hususani maeneo ya Dar es Salaam.

Leo tutaelekezana namna ya kuandaa supu hii nyumbani kwako na ikanoga ukaendelea kujilamba badala ya kunywa barabarani.

**Vipimo**

Pweza kilo moja, chumvi kijiko kimoja cha chai, tangawizi mbichi iliyosagwa kijiko kimoja cha chai, kitunguu saumu iliyosagwa na kijiko cha chai.

Mahitaji mengine ni masala ukipenda kijiko cha supu kimoja, pilipili mbuzi ili ipate kiharufu kizuri ikichemka, maembe mabichi na ndimu au limau kuchapuzia.

Namna ya kutengeneza

Osha pweza kisha mkatekate, mtie viungo vyote ulivyotayarisha na chumvi, mwache nusu saa akolee viungo na mtie ndani ya sufuria bila maji mfunike kisha weka jikoni, atatumbuka maji mwenyewe kwa moto wa kiasi paka awe rangi ya damu ya mzee (maroon).

Akishaiva kwa rangi hiyo ongeza maji weka na maembe yako yachemkie alafu tia kidimu au kilimau ichapukie hapo tayari kwa kula na wali na kuongeza afya ya mwili.





MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## Kioo chako kina hali gani?

**Na Restuta James**

KIOO ni moja ya pambo la ndani lenye 'ladha' ya kipekee kutokana na nguvu yake ya kubadili mwonekano wa eneo.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa kioo ni pambo ambalo limetumika kwa karne kadhaa bila kuchuja thamani yake.

Moja ya sifa ya kipekee ya kutumia kioo kama pambo ni uwezo wake wa kubadili mwonekano wa chumba kidogo kuwa kikubwa na kupunguza eneo kubwa kuwa la kawaida, kulingana na namna ya uwekaji.

Akizungumza na NIPASHE, mtaalamu wa mapambo ya ndani, Winnie Joseph, anasema kioo ni pambo linalowekwa sehemu tofauti tofauti kuanzia jikoni, sehemu ya kulia chakula, chumbani, koridoni na eneo la kuswakia.

Anasema pamoja na kwamba kioo kimezoeleka, iko njia ya kufurahia pambo hili la karne kadhaa kutokana na wataalamu kubadili mwonekano na ubora.

Winnie anasema hivi sasa kioo kimekuja na taa mahsusi huku kikiwa na teknolojia ya kuondoa ukungu kwa wale waliokiweka bafuni na kuoga kwa maji moto.

"Siyo tu hivyo, design (aina) mpya ya hili pambo imekuja na sehemu ambayo unaweza kuunganisha simu yako kupitia bluetooth na kusikiliza muziki unaoupenda huku ukioga au kujipaka mafuta," anasema.

Anasema vioo vilivyoboreshwa kwa uwezo huo ni vikubwa akigusia pia pambo la vioo vidogo, ambavyo vikiwekwa vingi sehemu moja vinavyoongeza mwonekano.





# Fanya uchaguzi sahihi wa sakafu ya nyumba

KILA uchao tunashuhudia mabadiliko yanayojitokeza maishani ambayo kwa namna tofauti yanasababishwa na maisha ya utandawazi tuliyo nayo katika karne ya leo.

Mambo yaliyofanyika jana si yale yanayofanyika kesho wala keshokutwa. Kila siku yanaibuliwa mapya au kwa mtindo mwingine au kwa ubora zaidi endapo yaliwahi kufanywa. Leo tunaangalia ubora uliopo sasa katika uwekaji wa sakafu ndani ya nyumba.

Katika nyumba, sakafu ni moja ya vitu vinavyochangia kupendezesha nyumba na hata pale inaposakafiwa kwa utaalamu mzuri.

Yako baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kusakafia nyumba. Msanifu Majengo, David Kashozi, anaeleza kuwa kabla ya kuweka sakafu, ni muhimu kuangalia rangi ya nyumba ili visipishane sana.



Jambo la pili ambalo anasema linapaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uchaguzi wa sakafu ni ubora wake na jambo la tatu ni kuchagua sakafu ambayo ni rafiki na salama kwa makundi yote ya watu wanaoishi katika nyumba yako.


"Chagua sakafu ambayo haitawakwaza baadhi ya watu kulingana na umri wao hususani watoto, wazee na wagonjwa, maana nyingine zina utelezi mkali," anasema Kashozi.

Jambo la nne, anasema ni vizuri kuzingatia kuchagua sakafu ambayo ni bora na inadumu kulingana na bajeti uliyojiwekea kabla ya kubadili nyingine.

"Japokuwa tunashauri kwamba usiwe nyuma ya wakati sana, hakikisha ni bora lakini inaendana na wakati," anasisitiza.

Na jambo la tano, anashauri kwamba ni vema kufanya maandalizi mapema ya aina ya sakafu unayoitaka.

# KATUNI




***KINYUNYIZO CHA LEO...**

KAMA SAA SIO MUHIMU CHELEWA UENDAKO

## HABARI KIMATAIFA



Wapiganaji wa kundi la Al Shabaab. **PICHA: BBC**

# Al Shabaab yafanya mashambulizi 9 wauawa

**MOGADISHU,** SOMALIA

POLISI nchini Somalia wamesema watu tisa wameuawa kwenye shambulio lililofanywa na wapiganaji wa kundi la Al Shabaab katika hoteli maarufu ya Pearl iliyopo ufukweni mwa jiji la Mogadishu.

Kundi hilo la Al shabaab limekiri kuhusika na shambulio hilo katika fukwe za mji mkuu wa Somalia, Mogadishu siku ya Ijumaa.

Miongoni mwa waliouawa katika hoteli ni raia sita na askari watatu, polisi wameeleza katika taarifa yao.

Mkurugenzi wa kampuni ya huduma ya magari ya wagonjwa ya Aamin, Abdikadir Abdirahman, amesema maofisa wake waliwabeba watu wapatao 20 waliojeruhiwa kutoka kwenye eneo la tukio.

Polisi imesema vikosi vya usalama viliwaokoa raia 84 na hadi sasa hatima ya washambuliaji waliohusika na shambulio hilo bado haijulikani.

Shirika la Habari la Kitaifa la Somalia limeandika kwenye ukurasa wake Twitter kwamba vikosi vya usalama vilifanikiwa kuwadhibiti wapiganaji wa al Shabaab waliohusika na shambulio hilo.

Jana Jumamosi uchafu ulionekana kutapakaa kwenye hoteli hiyo kutokana na shambulio lililotokea na vilionekana vioo vya madirisha vilivyovunjika pamoja na damu.

Hussein Mohamed, mhudumu anayefanya kazi katika hoteli nyingine iliyo karibu, amesema alisikia mlipuko uliofuatiwa na milio ya risasi wakati mashambulizi yalipoanza.

Kundi la Al-Shabaab lenye mafungamano na kundi la kigaidi la Al Qaeda limesema ndiyo limehusika na shambulio hilo, limeeleza wapiganaji wake walifanikiwa kuingia katika hoteli ya Pearl kupitia kwenye ufukwe.

Novemba jana kundi hilo ambalo linadhibiti baadhi ya maeneo ya nchi ya Somalia, wapiganaji wake waliishambulia hoteli nyingine maarufu ya Lido iliyo pia kwenye ufukwe wa bahari mjini Mogadishu, na kusababisha vifo vya watu tisa.

Awali Al Shabaab walidhibiti eneo kubwa la Somalia kabla ya kushindwa nguvu na kurudishwa nyuma katika operesheni zinazoendeshwa na vikosi vya serikali tangu mwaka jana.

Lakini wanamgambo hao bado wana uwezo wa kufanya mashambulizi dhidi ya sehemu muhimu za serikali, za kibiashara na hata za kijeshi.

Mwishoni mwa mwezi Mei, wapiganaji wa Al Shabaab walishambulia kambi ya kijeshi ya Bulo Marer waliyokuwepo wanajeshi wa Uganda wa kulinda amani wa kikosi cha Umoja wa Afrika.

Wanajeshi 54 waliuawa kwenye shambulio hilo lililofanyika umbali wa kilomita 130 kusini magharibi mwa jiji la Mogadishu.

# Papa Francis aendelea kupata nafuu baada ya upasuaji

**ROME,** ITALIA

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis anaendelea kupata nafuu baada ya kufanyiwa upasuaji.

Hata hivyo, Papa Francis, hatahudhuria misa ya leo Jumapili.

Kwa mujibu wa daktari wake, Sergio Alfieri Papa Francis anaendelea kupata nafuu baada ya kufanyiwa upasuaji wa utumbo na hana homa, na moyo wake pia unafanya kazi vizuri.

Lakini madaktari wamependekeza kutohudhuria sala ya leo Jumapili za umma kuepusha shinikizo katika misuli yake ya tumbo.

Daktari Alfieri amesema kwa kawaida baada ya upasuaji kama huo, mtu hulazwa hospitalini kwa kati ya siku nne na tano.

Alfieri ameongeza kuwa wanatumaini kumshinikiza papa kubaki hospitalini kwa wiki moja zaidi ili kumuwezesha kurejea kufanya kazi kwa nguvu zaidi na usalama lakini akasema uamuzi wa kutoka hospitalini ni wa papa mwenyewe.

## Wanaharakati wa Hong Kong waandamana Taiwan

**TAIPEI,** TAIWAN

MAMIA ya Wanaharakati, wanafunzi, na raia wa Hong Kong wanaoishi nchini Taiwan wameandamana katika barabara za jijini Taipei kuhimiza watu kuendelea kuunga mkono demokrasia na haki za binadamu huko Hong Kong.

Maandamano hayo yalifanyika kwa ushirikiano wa pamoja wa mashirika ya kitaifa na kimataifa yasiokuwa ya serikali ikiwa ni pamoja na kundi la raia wa Hong Kong wanaoishi Taiwan na shirika la Amnesty International kuadhimisha mwaka wa nne wa maandamano ya kuunga mkono demokrasia yaliohusisha mamilioni ya wakazi wa Hong Kong.

Licha ya mvua kubwa, washiriki wengine wakiwa wamevalia fulana nyeusi kama waandamanaji wa Hong Kong wa mwaka 2019, waliandamana katika eneo la kati la Taipei.

Inakadiriwa kwamba watu elfu moja walishiriki katika maandamano hayo.

Washirika hao walisema kuwa hawapaswi kusahau maandamano yaliyopita ya demokrasia mjini Hong Kong ama wanaharakati ambao kwasasa wamefungwa katika eneo hilo.

## Watu 5 wafariki kwenye kiwanda Uturuki

**ANKARA,** UTURUKI

MLIPUKO kwenye kiwanda cha kutengeneza roketi na vilipuzi nchini Uturuki umesababisha kuporomoka kwa jengo moja na kuwauwa wafanyakazi watano waliokuwa katika jengo hilo.

Kwa mujibu wa BBC mlipuko huo ulitokea katika saa za asubuhi kwenye kiwanja cha shirika la sekta ya mitambo na kemikali linalomilikiwa na serikali kwenye mji mkuu Ankara.

Shirika la habari la kibinafsi NTV limeripoti kuwa moshi wa kijivu ulionekana ukipaa kutoka kiwanja hicho huku magari ya wagonjwa na yale ya kuzima moto yakifika katika eneo hilo.

Jamaa za familia pia walifika katika eneo hilo kuwajulia wapendwa wao.

Mlipuko huo huenda ulisababishwa na mmenyuko wa kemikali wakati wa kutengeneza baruti na kwamba polisi wameanzisha uchunguzi rasmi wa tukio hilo.

MAKALA

# DHANA YA USHAWISHI NA MAMLAKA YA KIONGOZI



Na Magabilo Masambu

**Hata hivyo, kwa mujibu wa Mwanasaikolojia Berne Erick, uwezo wa ushawishi wa kiongozi unaweza kuathiriwa na aina nne za nafasi/himaya za maisha (Psychological Positions) kama ifuatavyo; Himaya ya kwanza ni mimi niko sawasawa; wewe uko sawasawa (I am OK; You are OK). Hii ni himaya ya maisha ambayo ni kamilifu na inaruhusu uwezo wa kufikiria sawasawa.**

KUNA mitazamo miwili tofauti ambayo watu mbalimbali wamekuwa nayo kuhusu viongozi. Wengine wanaamini mtu huzaliwa akiwa kiongozi na wengine huamini viongozi wanaandaliwa. Mitazamo yote inaweza kuwa sawa kutegemea mtu mwenyewe, lakini mazingira ya kisaikolojia hayatoi nafasi kubwa kwamba kiongozi anazaliwa akiwa kiongozi bali kiongozi huandaliwa.

Tunaweza kusema uongozi ni uwezo wa kushawishi. Kipimo kizuri cha uongozi bora si kutoa amri au kuonyesha mamlaka kwa wale unaowaongoza bali ni kushawishi watu wake, iwe kwa maneno, matendo au kwa kila aina ya tafsiri ambayo itawafanya kukubaliana naye katika maono yake.

Kiongozi katika taasisi anaweza kuwa na maono na mipango mizuri lakini anapokosa uwezo wa kushawishi juu ya maono na mipango yake, anaweza kukwama hata kama ni mazuri kiasi gani. Unaweza kuona kwamba ushawishi ni zaidi ya mamlaka kwa sababu mtu yeyote akishapewa uongozi moja kwa moja, anapewa na mamlaka lakini ushawishi hubakia kumtegemea kiongozi husika.

Hii ndiyo maana kiongozi yeyote lazima ahakikishe anakuwa na ushawishi kwa wale anayewaongoza la sivyo atalazimika kutumia nguvu kubwa kushinikiza maono yake yakubalike katika taasisi au jamii anayoiongoza. Kiongozi mzuri hujivunia zaidi nguvu yake ya kushawishi na si nguvu ya mamlaka aliyopewa.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Mwanasaikolojia Berne Erick, uwezo wa ushawishi wa kiongozi unaweza kuathiriwa na aina nne za nafasi/himaya za maisha (Psychological Positions) kama ifuatavyo; Himaya ya kwanza ni mimi niko sawasawa; wewe uko sawasawa (I am OK; You are OK). Hii ni himaya ya maisha ambayo ni kamilifu na inaruhusu uwezo wa kufikiria sawasawa.

Himaya hii hujengeka zaidi mtu anapopata kibali kwa wingi katika jamii (OK experiences). Watu wenye himaya hii ya maisha huonekana kujiamini na kuonyesha uwezo mkubwa katika kufanya kazi na hujisikia maisha ni kitu cha thamani.

Viongozi wenye himaya hii ya maisha wana sifa kuu tatu. Mosi, wana uwezo wa kutatua matatizo kwa ubunifu na kwa namna ya kujenga, pili ni wazuri sana katika kugawa majukumu na ni watendaji wazuri lakini sifa ya tatu wana uwezo wa kujali watu na kazi.

Himaya ya pili ni mimi niko sawasawa; wewe hauko sawasawa (I am OK; You are not OK). Himaya hii huonekana zaidi kwa watu wenye hisia kwamba wamekandamizwa, wameonewa au wamenyanyaswa. Watu hawa wamekutana na mazingira korofi au tabia korofi ya ama wazazi au walezi wao katika kipindi cha utoto. Ijapokuwa sasa ni watu wazima, wanaweza kuchukulia dunia kama adui zao.

Watu wa jinsi hii hulaumu wengine kwa matatizo yao na kamwe hawawezi kuamini wengine. Akitokea kuwa kiongozi mtu wa himaya hii ya maisha anakuwa mtu wa kujali kazi zaidi kuliko kitu chochote (task-oriented leader). Hawezi kujali hisia za wengine na kugawa majukumu kwake ni adhabu kubwa, hupendelea kufanya kila kitu mwenyewe.

Himaya ya tatu ni mimi siko sawasawa; wewe uko sawasawa (I am not OK; You are OK). Himaya hii ya maisha ni kwa watu ambao hujisikia kutokuwa na ushawishi wowote (powerless) akijilinganisha na wengine. Mtu kama huyu siku zote hulalamika na akiwa kiongozi hujali sana uhusiano kazini. Hisia zake ndiyo huamua matendo yake. Vilevile kiongozi kama huyu hatabiriki na hana mpangilio katika kazi zake.

Himaya ya nne ni mimi siko sawasawa; wewe hauko sawasawa (I am not OK; You are not OK). Hii ni himaya ya maisha kwa watu ambao wamekataliwa na wazazi wao na kulelewa na wengine. Mtu wa aina hii hujisikia ni mtu asiye na thamani na mara nyingi huwa na maamuzi ya kujidhuru au kudhuru wengine. Akiwa kiongozi hajali kazi wala uhusiano na hawezi kuwa maarufu kwa jambo lolote.

Kwa kuangalia aina hizo nne za himaya za maisha, unaweza kuona ulivyo umuhimu kwa wazazi na walezi kuwa makini katika malezi ya watoto wao, wakizingatia kuwa wana wajibu kuandaa watu ambao watakuwa viongozi wa kesho na ushawishi katika mambo yenye kuamua mustakabali wa taifa au jamii kwa ujumla.

Wazazi wana nafasi kubwa ya kukiandaa kizazi cha sasa kuja kuwa viongozi bora baadaye. Yaani wana wajibu wa kuwajenga watoto wao ili wakue wakijiamini na kutambua misingi, haki na wajibu wao katika jamii. Katika kutekeleza wajibu huu muhimu, lazima mzazi awe makini sana kwani vile utakavyomtendea mtoto akiwa mdogo, inaweza kuathiri nafasi yake ya ushawishi akija kuwa kiongozi baadaye.

Matokeo ya mtoto kulelewa katika mazingira ya kutokusikilizwa, yanaweza kuathiri uwezo wake wa kuwa kiongozi bora wa baadaye katika jamii au taasisi. Anaweza kuona kutosikiliza matatizo au kilio cha mtu mwingine ndiyo mpango mzima wa maisha kumbe ni kwa sababu tu amelelewa katika mazingira yasiyotoa kipaumbele katika kumsikiliza mtu mwingine.

**0689157789**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Wote ni abiria wangu, mimi ni taxi driver'



Na Adam Fungamwango

KWENYE dunia ya mahusiano, kitu kiitwacho wivu huwa hakikwepeki. Huko nyuma katika safu hii tuliwahi kueleza wivu ni kitu gani.

Tulisema wivu ni ubinafsi, wa mtu kutaka kumiliki kitu kuwa cha kwake mwenyewe na mwingine asikipate. Pia wivu ni tabia ya mtu kukasirika au kuchukia mtu mwingine anapopata kitu, cheo au jambo lolote zuri ambalo yeye alihitaji lakini hakuweza kulipata.

Mapenzi nayo ni hivyo hivyo. Yeyote anayekuwa na mpenzi, anataka awe wake peke yake na kusiwe na mwingine yeyote zaidi yake.

Ni hali ya kaiwada sana kwenye mapenzi. Wivu na mapenzi ni kama samaki na maji, lakini kuna aina ya wivu ambao unakera na kuwa usumbufu kiasi kwamba unakosesha raha na amani.

Unaweza kukuta mtu anampigia simu mpenzi wake lakini ikaonyesha kuwa anaongea na simu nyingine, basi hilo linakuwa ni tatizo kubwa.

Baadaye unakuwa ni ugomvi, bila kujua kuwa labda alikuwa anaongea na ndugu zake au wazazi wake. Na pia hata kama ni mpenzi wako, bado ana uhuru wa kuongea na watu wengine ambao ni marafiki zake na anaowafahamu. Ikifika huko sasa inakuwa siyo wivu ni karaha.

Kuna wanaume ambao hawataki hata wake zao kwenda kujumuika na wenzao kwenye hafla au sherehe mbalimbali. Wakati wanawake wenzake wanakusanyana kwenda harusini, au 'kicheni pati', kuna mwanaume anampiga marufuku mkewe kwenda kwa sababu akili yake inamtuma kuwa akiwa huko anaweza kukutana na wanaume wengine wakamrubuni.

Anashindwa kujua kuwa mkewe ana akili timamu, na kwamba kama kurubuniwa inawezekana kabisa hata akiwa nyumbani hapo inawezekana wakaja watu kumrubuni pia.

Kuna wivu wa kawaida na mwingine unaleta hasara kwa sababu wapo ambao hawataki hata wake zao kujishughulisha na uzalishaji mali, kama vile kufanya kazi, au biashara.

Na hana lolote analomkatazia ni wivu tu. Ndiyo maana bendi ya Kurugenzi Jazz ya Arusha katikati ya miaka ya 1970, ilitunga wimbo waliouita'Wivu', wakiwatuhumu akinababa wanaowakatalia wake zao kufanya kazi au biashara.

"Wivu ukizidi nyumbani mapenzi yapungua, wivu usio na maana waleta hasara.

Umepata kitu gani bibi umepata kitu gani, bibi umemkataza kufanya kazi, eti sababu achelewa nyumbani Matatizo mengi sasa yakukuta, mahitaji washindwa kumtekelezea."

Jamaa anamchana mwenzake aliyemkataza mkewe asifanye kazi, kilichotokea ni kwamba nyumbani kuna matatizo na mahitaji ya muhimu anashindwa kumtekelezea.

"Wivu ukizidi nyumbani hasara, matokeo yake ni kutoamiana. Wivu unaleta ugonjwa wa moyo, sababu ya kuweka mke rohoni. Tuliza moyo kijana waache wake zenu waende kazini mama."

Anazidi kumwambia kuwa wivu ukizidi ni hasara kwa sababu kinachotokea ni kutoamiana. Unaleta ugonjwa wa moyo kwa sababu ya kuweka mke rohoni.

Ni kwamba kila anapokuwa nje ya nyumbani unakuwa na wasiwasi na kupiga simu kumuuliza yuko wapi. Kwa hali ya kawaida hakuna binadamu ambaye anaweza kufurahia hilo, iwe mke au mume. Ina maana humuamini, kitu ambacho wengi hawakipendi.

"Kina baba wivu haufai jana, wivu siyo dawa, waruhusuni waende kazini wake zenu, wakafanye kazi.

Maisha ya leo ni kufanya kazi, mke na mume kusaidiana."

Tukija kwa akinamama nao wapo wenye tabia hiyo. Mwanaume anachelewa kwa sababu za kikazi, anarudi nyumbani akiwa hoi amechoka, lakini ataangaliwa kwa jicho baya na atamaliziwa na neno, 'ndiyo unarudi saa hizi?"

Kabla mwanaume hajajibu, anaweza kusikia tena sauti ya mkewe "ulipitia kwa hawara yako?" Hapo mwanaume huchoka zaidi kwa sababu yote anayoyafanya ni kwa ajili ya familia yake, lakini hapati ushirikiano wowote, badala yake kushutumiwa kuwa anachelewa kurudi nyumbani.

Mwanaume anajiuliza, hivi angemkataliwa bosi wake kwa sababu tu awahi kurudi nyumbani? Pamoja na kwamba anampenda mkewe na watoto wake na anahitaji kukaa na familia yake, lakini akiwa hana kazi anaweza kuwa na furaha na hiyo familia.

Hapo mwauame anaona ni bora tu aendelee kupigwa madongo, lakini ataendelea kuheshimu maagizo ya kazini kuliko ya mkewe. Na wakati mwingine anamsamehe tu mkewe kwa kile ambacho anaona hajui atendalo.

Siku akimaliza kazi mapema, mwanaume anaamua kuwahi nyumbani ili akae na familia yake. Anapoaingia, mkewe anaonekana kushangaa kwa mumewe kurejea mapema.

Mume yeye mawazo yake anadhani atapokelewa kwa bashasha, kinyume chake anaangaliwa kwa kebehi, halafu naambiwa "hawara yako leo hayupo nini? Mbona umerudi mapema hivyo!" Yaani hakuna kizuri, ukirudi mapema tabu, ukichelewa shida.

Kuna kisa kimoja hivi ambacho kilitungiwa wimbo na DDC Mlimani Park Orchestra kinachohusu mke kumshutumu mume kuwa na wanawake wengi kwa sababu tu ni dereva taxi.

Mke anadhani au anaambiwa na wambeya kuwa anaowabeba ndani ya gari baadhi yao si wateja, ila ni mabibi zake. Kwa hali ya kawaida amsafirishaji abiria awe dereva taxi, bodaboda au bajaj, huwa hachagui abiria, Mrefu, mfupi, mzee, kijana, mwanaume, mwanamke, wote hao ni abiria zake, ili mradi tu walipe nauli.

Mume baada ya kulifahamu hilo, anakwenda kwa mkewe na kumwambia ukweli kuhusu hilo, na kumtaka asiwe anasikiliza maneno ya watu. Wimbo huu unaitwa 'Taxi Driver', ambao Sikinde Ngoma ya Ukae waliurekodi miaka ya 1980.

"Mama Jackline, ninajua ni nini kiachokunyima raha oo, mama Jackline, ninajua ni nini ninachokukondesha. Usijipe tabu mama moyoni mwake, kwa maneno ya kuambiwa mama ooo Jackline. Kazi yangu isiwe ndiyo sababu au kisingizio, kuwa gari langu si taxi bali gari la kubeba vimada. Usisahau abiria wangu si wa aina moja, awe mwanaume awe mwanamke, wote ni abiria wangu ee, mimi ni taxi driver.'

Wimbo huu ilitungwa na mpiga solo, Joseph Mulenga, unatoa fundisho kwa wapenzi au wanandoa kuacha wivu usio na kichwa wala miguu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-14

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

SASA kila mtu alielewa tatizo lilikuwa ni nini. Lakini bado wengi walikuwa na maswali ya kujiuliza. Wanawake hao waliogombana hadi kusababisha jambo hilo ni kina nani? Na Ilikuwaje hadi kutukanwa asiyehusika, na kwa nini Husna hakugundua kama simu ile haikuwa ya kwake baada ya kukoga matusi?

"Nimezungumza sana, kwa bahati nzuri tumefanya kila kitu sisi.

Tumemualika dada ambaye simu yake ilibadishwa na akapewa Husna na ya Husna kupewa yeye.

Atasimama mtamuona, na sikutaka kulitaja jina lake kabla, yeye mwenyewe atajitambulisha."

Massawe baada ya kusimama na kuzungumza kwa muda mrefu, aliketi.

Badala yake akasimama dada mmoja mwembamba mrefu, mweupe mwenye pua iliyochongoka. Mavazi yake aliyovaa na alivyojipamba maalum kwa ajili ya hafla hiyo ilikuwa kivutio tosha.

Alipendeza kutokana na muonekano wake.

Macho yake makubwa yaliyoonekana kama anasinzia, yalionyesha kuwa na aibu.

Wote walikuwa na shauku kujua ataongea nini.


"Samahani jamani, mimi sio muongeaji sana, kwa hiyo mengine mtanisamehe tu. Yaani sijui nianzie wapi?"

"Anzia hapo hapo." Ilisikika sauti moja ya kiume, lakini ikionyesha kabisa kuwa alikuwa ameutwika. Kichofuatia ni vicheko.

"Mimi naitwa Pendo, ni mke wa bwana Paul, kwa bahati mbaya yeye ana udhuru ilikuwa anisindikize hapa. Mimi pia ni mgeni mualikwa hapa na walionialika si watu ambao nawafahamu sana, nao ni Bello na Massawe. Mimi nina miezi miwili na nusu tangu niolewe, nilipoolewa tu bado mgeni kabisa nikapata shoga 'angu mmoja akanipasha kuwa kabla sijaolewa mimi mume wangu alikuwa anatembea na msichana mmoja hapo jirani.

Msichana huyo alipelekwa hadi kwa ndugu za mume wangu na kila mtu akawa anamfahamu, kila mmoja akajua yeye ndiye ataolewa. Mimi sijui kilichotokea, lakini leo hii nimeolewa mimi.

Sababu sijajua, mimi sikuwepo. Kwa hiyo shoga 'angu huyo akaniambia niwe makini kwa sababu ananitafuta na anaulizia hadi namba zangu ili anitukane na kunitisha. Kisa eti mimi nimesababisha yeye asiolewe.




**Mimi sijui kilichotokea, lakini leo hii nimeolewa mimi. Sababu sijajua, mimi sikuwepo. Kwa hiyo shoga 'angu huyo akaniambia niwe makini kwa sababu ananitafuta na anaulizia hadi namba zangu ili anitukane na kunitisha. Kisa eti mimi nimesababisha yeye asiolewe.**

Siku moja nasikia simu inaita, nilipopokea, nikaanza kupakiwa matusi na mwanamke ambaye alijitambulisha kuwa ni mpenzi wa mume wangu.

Nikajua ni yeye yule yule niliyeambia na shoga 'angu alivyoniambia, mimi sikuwa na muda, nikaikata na kuzima simu yenyewe."

Stori hiyo ikamvutia na kumpendeza Husna kwa sababu na yeye yamemkuta.

Na tayari alishaanza kugundua kuwa nani alimpigia simu siku ile.

"Kwa bahati mbaya au nzuri baadaye wakati nataka kuichukua juu ya meza, ikateleza na kuanguka chini.

Haikuwaka tena, ikabidi niipeleke kwa fundi. Fundi mwenyewe ndiyo huyu hapa Massawe.

Ikakaa huko, ikalala kwa sababu sikuwa na pesa, kesho yake jioni nikapata pesa, nikaenda kuigomboa. Niliporudi nayo nyumbani kuiwasha ikawaka, ila sasa baada ya muda wakawa wanapiga watu ambao siwafahamu, baadaye nikaja kugundua kuwa haikuwa simu yangu, nimepewa simu ya mtu mwingine ila zinafanana kila kitu, zote zimetengenezwa na kampuni moja ni aina moja na rangi vile vile.

Kesho yake tena asubuhi nikairudisha kwa fundi, kufika kafunga, nilipouliza wakaniambia amesafiri kwenda Moshi amefiwa na baba yake mzazi.

Nilirudi nyumbani nikamueleza mume wangu, akanishauri nikasajili laini nyingine akanipa simu yake nyingine nitumie mpaka Massawe atakaporudi."

Umakini wa kila mtu alizidi kuongezeka kusikiliza mkasa huo wa kusisimua. Dan na Husna ambao walikaa tofauti kabisa walisisimkwa zaidi.

"Baada ya mwezi hivi na siku chache kupita, alirudi nikaenda na ile simu nikamwambia hii si ya kwangu umenibadilishia.

Kweli alikubali, lakini akasema simu yangu ameibadilisha kwa kumpa mteja mwingine, lakini imesababisha watengane na mumewe kwa sababu kuna mwanamke amempigia simu na kujitambulisha ni hawara ya mumewe, mke kapaniki kaamua kuondoka nyumbani.

Nikamwambia fundi hiyo simu ya matusi ilikuwa ya kwangu hiyo, kuna dada pale nyumbani ananitafuta na huyo ndiye aliyempigia, nia yake ilikuwa ni mimi, ila simu zimebadilishwa."

Pendo aliendelea kufunguka na kisa hicho kilisababisha watu kusahau kama juu ya meza kuna vinywaji, akili na macho yake yakiwa kwa Pendo.

"Siku tatu baadaye nilipokwenda tena ofisini kwa Massawe, nilimkuta ana mtu mwingine ambaye ndiyo huyu aliyetualika hapa kwenye hii sherehe, Belo.

Akaniambia kuwa simu yangu imebadilishwa na ya shemeji yake, na imewafanya watengane na mdogo wake, lakini wakanitaka mimi nwasaidie ili mke wa mdogo wake aamini kuwa haikuwa ni simu ya hawara wa mumewe.

Nikawauliza sasa mimi niwasaidia vipi? Wakasema hili tukio ni lazima mimi na huyo aliyepiga simu kunitukana mimi tuwepo na tuthibitishe mbele ya shemeji yake la sivyo itakuwa ni vigumu sana kama wao watakwenda kuongea maneno hayo wakaaminika.

Akasema shemeji yake anaweza kadhani ni mpango tu na stori ya kutungwa imetengenezwa ili amrudie mumewe. Na mimi nikawaza, nikaona kweli, tayari simu aliyonipigia yule mpenzi wa zamani wa mume wangu imeleta balaa kwenye ndoa nyingine, na mimi ni mwanamke, na ukweli naujua, huko mwanamke mwenzangu anateseka na ndoa kwa sababu ya kitu ambacho si kwa kweli na mimi naweza kuthibitisha, nikakubali."

Akashusha pumzi kidogo na kutoa kikohozi chepesi. Ilionekana sasa siyo pati tena, bali kumegeuka kuwa na kikao cha kifamilia.

"Wakaniuliza tutampataje huyo aliyekupigia simu, nikawaambia yupo tu pale mtaani kwetu na namfahamu.

Wakaniomba niwapeleke. Kwa bahati nzuri niwaambei tu ugomvi wangu na yeye umekwisha, alivyopata na yeye mchumba akaja kuniomba radhi, siku si nyingi na yeye ataolewa.

Nikawapeleka kwake, tukayazungumza, tukakubaliana na ndiyo Belo akaandaa huu mpango wa pati hii ili kupata fursa ya sisi kuueleza hapa kila mtu aelewe na wasioamini waamini. Mimi nimemaliza ya kwangu."

Belo akasimama, akamkaribisha mwanamke mwingine. Huyu ndiye aliyepiga simu kumchamba Pendo, lakini simu tayari alikuwa ameshabadilishwa, ipo kwa Husna."

ITAENDELEA JUMAPILI

# 50 CENT APATA PESA KIDUCHU FILAMU YA 'POWER'

Rapa, na mwigizaji 50 Cent amesema alipata pesa kidogo tu alipojitosa kwa mara ya kwanza kuigiza filamu ya 'Power'.

Msanii huyo ambaye jina lake halisi ni Curtis James Jackson amesema

"Nililipwa dola chache ili kuigiza na niliwapa wimbo wa mandhari ya Power, nilikubali kwa sababu ya kufanya shoo iwe nzuri sana."

Alisema hadhani kama kuna mtu yeyote staa ambaye angeweza kukubali pesa aliyokuwa akilipwa, lakini yeye alifanya hivyo na sasa anakula matunda yake.

Kwa sasa anasema ametengeneza zaidi ya matoleo 20 ya filamu hiyo inayoonyeshwa kwenye shoo za TV kama tamthilia, na zinazofadhiliwa na watu aliokutana nao alipokuwa akisafiri ambao walitaka kuwekeza matangazo yao kwenye 'episodi' mbali mbali hatimaye pesa za maana zikaanza kuingia na analipwa pesa nzuri.

"Nikaanza kukusanya dola milioni $200 (zaidi ya Tsh Billion 400) na mwishowe, tukaanza kuingiza dola milioni 10 kwa kila 'episodi' tunazotoa, sasa nalipwa vizuri" alisema msanii huyo.





# Lavalava aja na ngoma mpya

Msanii kutoka lebo ya WCB, Lavalava, ametangaza ujio wa ngoma mpya Jumatano ijayo baada ya kimya kirefu.

Mara ya mwisho ilikuwa ni Julai 28 mwaka huu, alipotoa ngoma iitwayo 'Desh Desh', ambayo baadhi ya mashabiki walitabiri itakuwa ni ya mwisho kwake kabla ya kuondoka chini ya lebo hiyo.

Msanii huyo kwenye mtandao wake wa kijamii, ameandika kuwaita mashabiki zake mara tatu. "Mashabiki zangu, mashabiki zangu, mashabiki zangu. Nimewaita mara tatu, hiyo tarehe 14/4/2023, nakuja kuua mtu." akaandika msanii huyo.

Mashabiki wa Lavalava wamepokea kwa furaha sana ujio wa ngoma hiyo ambayo jina lake bado halijatajwa, kwani wamekuwa wakilalamika sana juu ya msanii huyo kukaa muda mrefu bila kutoa ngoma yoyote.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**ROWE AWINDWA**
KLABU ya West Ham inavutiwa na dili linalomhusisha mchezaji wa Arsenal, Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 22, ikiwa kiungo mwenza wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24, atajiunga na Washikabunduki hao. (***Sun***)

**ALVAREZ DAU JUU**
KLABU ya Ajax inadai pauni milioni 45 kwa kiungo wao wa kati wa Mexico, Edson Alvarez mwenye umri wa miaka 25, ambaye ameibuka kama mbadala kwa West Ham kuchukua nafasi ya Declan Rice. (***Guardian***)

**BAYERN WAJITOSA**
BAYERN Munich inamtaka kiungo wa kati wa klabu ya West Ham, Declan Rice lakini hawajafanya lolote katika siku za hivi karibuni na Arsenal wanapigiwa upatu kumsajili. (***Sky Sport Germany***)

**GVARDIOL ATAKIWA CITY**
MANCHESTER City imefanya mazungumzo ya awali na klabu ya RB Leipzig kuhusu usajili wa mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 21. (***Football Insider***)

**CANCELO SAFI ARSENAL**
MAZUNGUMZO kati ya Arsenal na Joao Cancelo kuhusu uwezekano wa uhamisho wake yanaendelea vyema na Manchester City wanataka pauni milioni 45 kumuuza beki huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 29. (***Football Transfers***)

**LINDELOF HAUZWI**
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amezuia majaribio ya Eintracht Frankfurt kumsajili Victor Lindelof msimu huu wa joto, akisema beki huyo wa Sweden mwenye umri wa miaka 28 hawezi kuguswa. (***Bild, via Metro***)

**LAVIA AWANIWA**
CHELSEA imeanza mazungumzo na Southampton kumhusu kiungo wao wa Ubelgiji, Romeo Lavia mwenye umri wa miaka 19. (***Football London***)

**ONANA BADO HAKIJAELEWEKA**
GOLIKIPA wa Inter Milan raia wa Cameroon, Andre Onana amefikia makubaliano ya kimsingi na Chelsea lakini Inter wamekataa dau la awali la pauni milioni 34 The Blues kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. (***Tuttomercatoweb***)

**MAIGNAN ATAKIWA**
CHELSEA pia wanavutiwa na kipa wa AC Milan na Ufaransa, Mike Maignan mwenye umri wa miaka 27. (***L'Equipe***)

**BEGOVIC AWANIWA LUTON**
KLABU ya Luton Town imefanya mazungumzo na golikipa wa Bosnia, Asmir Begovic mwenye umri wa miaka 35, ambaye ameondoka Everton - na pia wanamfuatilia mlinda mlango wa Bournemouth wa Jamhuri ya Ireland, Mark Travers mwenye umri wa miaka 24. (***Telegraph***)

**LOFTUS-CHEEK NA CHELSEA**
CHELSEA inasubiri kuona kama AC Milan itatoa kiasi cha pauni milioni 15 kwa kiungo wao England, Ruben Loftus-Cheek mwenye umri wa miaka 27, baada ya kuwatimua wakurugenzi Paolo Maldini na Frederic Massara. (***Telegraph***)

**MAHREZ KUTUA ARABUNI**
KLABU ya Saudia Al-Ahli iko tayari kumpa winga wa Algeria, Riyad Mahrez mwenye umri wa miaka 32 mkataba wa thamani ya pauni milioni 40 kwa mwaka akiondoka Manchester City msimu huu wa joto. (***Mirror***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POGBA KUTIMKIA UARABUNI

## ●●● Atajwa kuondoka na nyota kibao Ulaya, huku Juventus ikiwa tayari...

**TURIN,** Italia

KIUNGO wa kati wa Juventus, Paul Pogba ndiye anayelengwa hivi sasa kwenye Ligi Kuu ya Saudi Arabia, kwa mujibu wa 90min.

Karim Benzema aliondoka Real Madrid na kujiunga na Al Ittihad Jumanne kwa mkataba wa miaka mitatu na N'Golo Kante anakaribia kujiunga naye, na kunatarajiwa kuwa na wimbi la wachezaji wenye majina makubwa ambao watafuata mkondo wao kwa kuungana na Cristiano Ronaldo Mashariki ya Kati.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alikuwa na msimu mbaya baada ya kurejea Juventus msimu uliopita wa joto kutoka Manchester United.

**Mfaransa huyo alianza mechi moja pekee ya Serie A msimu uliopita, huku akiondolewa kwenye kikosi cha Juventus kwa ajili ya mechi yao ya mtoano ya Ligi ya Europa dhidi ya Freiburg kwa sababu ya masuala ya kinidhamu.**

Licha ya ugumu wake, Pogba amesisitiza kwamba anataka kubaki Turin na kuthibitisha thamani yake, lakini Juve wenyewe wamevumilia kampeni ya misukosuko iliyokumbwa na migogoro ya nje ya uwanja.

Juventus sasa wanaangalia uwezekano wa kujengwa upya msimu huu wa joto - watacheza mechi ya kufuzu kwa Ligi ya Europa Conference mwaka ujao baada ya kukosa kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi ya Europa - na hilo linaweza kusababisha uwezekano wa kuondoka kwa Pogba.

Wachezaji wote wenye majina makubwa waliosajiliwa kufikia sasa ni uhamisho wa bure lakini Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji wa Umma (PIF), ambao pia wanamiliki Newcastle United, ukitoa fedha kwa klabu vinne bora za Pro League - Al Ittihad, Al Ahli, Al Nassr na Al Hilal - hawatakuwa na matatizo katika kulipa ada kubwa kwa malengo yoyote yajayo.

## Suarez kumfuata Messi Marekani

**NEW YORK,** Marekani

LUIS Suarez anatarajiwa kujiunga na Inter Miami pamoja na wachezaji wenzake wa zamani wa Barcelona, Lionel Messi na Sergio Busquets, kwa mujibu wa ESPN.

Jumatano Lionel Messi alithibitisha kujiunga na Inter Miami msimu huu wa joto, ambapo aataungana na rafiki wa karibu Sergio Busquets.

Na sasa nyota mkongwe wa Uruguay Suarez, ambaye alikuwa karibu sana na Messi pale Camp Nou, pia atajiunga na kikosi hicho kinachoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, MSL.

Messi anatua huko kwa uhamisho wa bure baada ya kumaliza mkataba wake na Paris Saint-Germain, na vile vile Busquets anakwenda bila malipo baada ya kuondoka Barcelona mwishoni mwa msimu wa Ulaya wa 2022/23.

Suarez amekuwa na klabu ya Gremio ya Brazil tangu mwaka jana baada ya kuitumikia klabu ya Nacional nchini kwao.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 ana mkataba na Gremio hadi mwaka 2024, lakini ana kifungu cha kutolewa ambacho yeye na Miami wameanzisha na usajili wake utathibitishwa hivi karibuni.

Kuwasili kwa Suarez kusini mwa Florida kutamaanisha kurejea kwenye kikosi sawa na Messi na Busquets kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2020, alipoondoka Camp Nou na kuelekea Atletico Madrid.

Watatu hao walikaa pamoja kwa miaka sita yenye mafanikio makubwa kule Katalunya na inaaminika kuwa Messi ametekeleza jukumu lake katika kusaidia kuwaleta wachezaji wenzake wa zamani kwenye klabu hiyo.




# MARTINEZ AWANIWA REAL MADRID, CHELSEA



**MILAN,** Italia

KLABU za Real Madrid, Chelsea na Manchester United zote zimetajwa kuwania kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez, ambaye anatarajiwa kuondoka Italia baada ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya jana Jumamosi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekuwa na msimu bora wa maisha yake ya Inter, akipachika mabao 21 na kutoa pasi saba za mabao kwenye Serie A.

Kwa mujibu wa 90 minutes wawakilishi wa Muargentina huyo wamezungumza na klabu kadhaa kuziarifu kwamba Martinez yuko tayari kwa changamoto mpya msimu huu wa joto.

Chelsea na United, ambazo zimekuwa zikifuatilia maisha ya Martinez kwa miaka mingi sasa, zimeonesha nia ya kutaka kumsajili, lakini italazimika kuzuia nia ya Real Madrid kama ikiwa wanataka kumleta kwenye Ligi Kuu England.

Hata hivyo, Real Madrid imeongeza nia yao katika siku za hivi karibuni huku wakijiandaa kwa marekebisho makubwa katika safu ya ushambuliaji.

Karim Benzema, Eden Hazard, Marco Asensio na Mariano Diaz wote wanaondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto, na kuwaacha Real Madrid wakiwinda wachezaji wengine muhimu.

Mchezaji wa Chelsea Kai Havertz anazingatiwa lakini wasiwasi juu ya bei yake inaweza kuzuia kusajiliwa.

Mshambuliaji anayelengwa na Real Madrid ni Harry Kane wa Tottenham Hotspur, ambaye pia ni kinara wa orodha ya wachezaji wanaotakiwa na Man United.

Spurs wamedhamiria kutomuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa England msimu huu wa joto, na hivyo kulazimisha klabu zote mbili kutafuta mahali pengine.

Kwa hiyo, klabu hizo mbili zinachunguza chaguzi zao zote na Martinez, ambaye Inter wanatarajia kuondoka katika klabu baada ya fainali ya Ligi ya Mabingwa, anaibuka kama shabaha nzuri sio tu kwa United na Real Madrid, lakini pia kwa Chelsea.

Kikosi cha Mauricio Pochettino, ambacho kinafuatilia hali ya Kane katika kutafuta mshambuliaji mpya, kiko kwenye mawasiliano ya mara kwa mara na Inter kuhusu masuala mbalimbali, ambayo ni mustakabali wa Romelu Lukaku na kutaka kumnunua kipa Andre Onana.

# Keita atua Werder Bremen

**LONDON,** England

KIUNGO wa zamani wa Liverpool, Naby Keita amerejea Ujerumani kujiunga na Werder Bremen baada ya kumalizika kwa mkataba wake pale Anfield.

Uhamisho wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Guinea wa pauni milioni 52 kwenda Merseyside kutoka RB Leipzig mwaka 2018 ulikuja na matarajio makubwa.

Hata hivyo, alikatishwa tamaa katika mechi zake 129 katika kipindi cha miaka mitano huku akijitahidi kukabiliana na hali ya Ligi Kuu ya England na kukosa muda mwingi kutokana na majeraha kadhaa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alicheza mara 13 pekee msimu uliopita, aliachwa nje ya kikosi cha Ligi ya Mabingwa Ulaya kutokana na jeraha, na alianza mechi tatu pekee za Ligi Kuu England.

Bremen watatumaini kurejea kwa kiungo huyo kwenye Bundesliga kutaleta mabadiliko ya bahati baada ya kufunga mabao 14 na kutoa pasi 14 za mabao katika mechi 58 za Leipzig kabla ya kuhamia Liverpool.

"Klabu kadhaa bila shaka vitavutiwa wakati mchezaji kama Naby Keita anapatikana kwa uhamisho wa bure," alisema mkuu wa skauti wa Bremen, Clemens Fritz.

"Kwa hiyo tunafurahi sana kwamba Naby ameamua kujiunga na Werder, licha ya ofa zingine kadhaa. Sifa zake zitaimarisha sana timu yetu."



# TWIGA STARS, COPPERS QUEENS MAJARIBUNI LEO

**Na Somoe Ng'itu,** LUSAKA

TIMU ya soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), inatarajia kuvaana na wenyeji Zambia (Copper Queens) katika mechi ya kirafiki na kimataifa itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Wpodlands jijini hapa.

Copper Queens imewaalika Twiga Stars ili kujipima kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Kombe la Dunia la Wanawake litakalofanyika kwa pamoja katika nchi za Newzealand na Australia.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, alisema mechi hiyo ni kipimo kizuri kwa timu yake ambayo pia imeanza maandalizi kuelekea kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (AWCON).

Shime alisema anaamini mechi itakuwa na ushindani kwa sababu ya historia ya timu hizi mbili kila wanapokutana katika mashindano mbalimbal.

" Utakuwa mchezo mzuri na wenye ushindani, tumefuraho kupata nafasi hii ya kuwapa changamoto Zambia, tunajuana, naamini kila upande utapata faida kupitia mechi hii ya kirafiki," alisema Shime.

Nahodha wa Twiga Stars, Amina Ally, alisema wamejiandaa vizuri kupambana na Copper Queens na anaamini watafanya vyema na watautumia mchezo huu kuendelea kujiimarisha.

"Ni kipimo kizuri sana kwetu, tumekuja kuonyesha ubora wetu, naamini wao pia walituchagua sisi kwa sababu wanaamini tutawasaidia kuwaweka imara kuelekea fainali za Kombe la Dunia," alisema kiungo huyo anayeichezea Yanga Princess ya Dar es Salaam.

Bruce Mwape, Kocha Mkuu wa Copper Queens alisema amekiandaa vyema kikosi chake kuelekea fainali za dunia na anaamini Twiga Stars itawapa maandalizi yatakayowasaidia kwenda kupeperusha vyema bendera ya Afrika katika michuano hiyo.

Mwape alisema wachezaji wake wako tayari na mashindano hayo na wanaamini watafanya vyema kutokana na kufanya maboresho mbalimbali.

"Tuko tayari kwa mechi ya kesho (leo) dhidi ya Tanzania, tunahitaji kupata ushindi ili kuifanya safari yetu kuelekea Kombe la Dunia kuanza vyema, tunajua utakuwa mchezo mgumu lakini tuko tayari kuwakabili, tuko tayari na fainali za Kombe la Dunia,"alisema Barbara Banda, nahodha wa Copper Queens.



Vijana wanaolelewa katika kituo cha kukuza vipaji cha Jakaya Kikwete (JMK Park), wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya kituo hicho jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Rais Zanzibar kuandamana na timu Olimpiki*

**Na Saada Akida**

RAIS wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi atakuwa sehemu ya msafara wa timu ya Taifa ya Olimpiki Maalum inayotarajia kushiriki Mashindano ya Dunia kuanzia Juni 17 Hadi 25 mwaka huu nchini Ujerumani.

Akizungumza na Nipashe jana, katika hafla ya kukabidhi bendera timu hiyo, Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Pindi Hazara Chana alisema Rais Mwinyi na baadhi ya viongozi watakwenda kuongeza hamasa kwa vijana hao.

Alisema kwenda kwa viongozi hao nchini humo ni sehemu ya kuisapoti timu hiyo inapeperusha vema bendera ya Taifa na kutwaa ubingwa.

"Wachezaji waende kupambana na kupata matokeo mazuri katika kila mechi, tumewaandalia mazingira ya timu yetu kwenda kushindana na kurudi na ushindi, tunaimani kubwa na vijana wetu kufikia kile tunachokitarajia," alisema Chana.

Naye Kamishna wa Idara ya Michezo Zanzibar, Ameir Makame alisema uwepo wa viongozi hao utasaidia kutoa hamasa ya ubingwa.

Kwa upande wa Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha alisema serikali imetoa Sh. milioni 50 kwa ajili ya maandalizi ya timu hiyo.

Timu hiyo ina wachezaji 20 wa mpira wa wavu na riadha kati ya hao 10 wanawake na 10 wanaume.

Timu hiyo ipo, chini ya makocha, Deogratius Zavery Mdemu kutoka Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Stephen Oloo kutoka Kigamboni na Augustino Shamte Mohamed kutoka Arusha.

## Mgunda: Tutalipa deni msimu ujao

INATOKA UK. 24

Akizungumza na Nipashe jana, Mgunda alisema kabla ya kucheza mechi ya mwisho ya ligi dhidi ya Dodoma Jiji, walikaa na Robertinho ili kufanya tathimini ya kikosi pamoja na wachezaji ambao wataendelea kusalia ndani ya timu kwa ajili ya msimu mpya.

Alisema msimu wa 2022/23 haukuwa na mafanikio kwao, kwani hawakufikia malengo yao licha ya wachezaji wao kufanya kazi nzuri uwanjani na kuifanya Simba kuwa timu inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya mabao ya kufunga.

"Tumefanya tathimini ya timu hatukufanikiwa kufikia malengo yetu kwa asilimia 100, lakini tumeweza kufika nusu yake, tumeshakaa na Robertinho kuona wapi tulipokosea msimu huu, tunajipanga upya kwa msimu ujao ambao kwetu unadeni kubwa kwa mashabiki wetu," alisema Mgunda.

Alisema baada ya kukabidhi mapendekezo hayo ana imani uongozi utafanyia kazi kwa kuboresha kikosi cha timu yao kuelekea mashindano ya msimu ujao.

"Nina imani hakutakuwa na maboresho makubwa kwa sababu ya Simba ina wachezaji wazuri na tunaongeza wale ambao watakuja kushirikiana na watakaosalia kikosini kwa ajili ya msimu mpya wa 2022/23." alisema Mgunda.

Kuhusu kiungo mshambuliaji wao, Saido Ntibazonkiza, Mgunda alisema ni mchezaji mzuri mwenye uwezo wa kusababisha na kuweza kufunga, jambo ambalo limeweza kumfanya kuingia katika kinyang'anyiro cha kuwania kiatu cha ufungaji bora.

"Ukiangalia msimu huu licha ya kushindwa kutwaa mataji lakini katika orodha ya ufungaji tumeweza kuongoza kuwa na idadi kubwa kuliko timu yoyote. Hivyo hili ni deni kubwa kwetu kwa sababu tunatakiwa msimu wa 2023/24 kuhakikisha tunatwaa mataji hayo na kuendelea kuongoza katika ufungaji," alisema kocha huyo anayedai msimu ujao wanakuja kivingine baada ya kufanya maboresho ya kikosi cha timu hiyo.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally amewataka mashabiki kuwatoyumbishwa na tetesi za usajili ambazo zinachochea migogoro baini yao na viongozi.

Alisema mashabiki na wanachama wanatakiwa kuwa makini na kutulia kwa tetesi watakazozipata, wanaandaa timu kubwa isiyofanana na ligi kuu Tanzania bali kikosi imara kinachokwenda kucheza michuano ya Super League.

"Kuna wachezaji tutaachana nao na kuwapa nafasi ya kwenda kutafuta changamoto zingine hasa kulingana mwaka huu tuna mashindano mengi, ikiwemo Super League," alisema Ally.

"Lazima tufanye usajili kulingana na mahitaji makubwa hatutaki kuingia na kuondolewa katika mchezo mmoja, lazima tufanye usajili mkubwa kulingana na ukubwa wa mashindano hayo, tunatoa fedha ya usajili kuleta wachezaji ambao watakuja kucheza michuano hiyo itakayoanza Agosti, lakini ndio hao hao watakaocheza na ligi," alisema Ahmed.

Kiungo Mshambuliaji, Saido alisema anafurahi kuona mashabiki wa Simba wakimuunga mko katika kinyang'anyiro cha kuwania ufungaji bora jambo ambalo kwake anawashukuru wachezaji wenzake kwa sapoti kubwa.

Alisema anafurahi kuwa sehemu ya kuwania tuzo ya ufungaji bora na kumpongeza mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele kumpa changamoto hiyo na ana imani ni mchezaji mzuri.

"Kwa msimu ujao tutafanya vizuri nina imani uongozi utakuwa tayari umeshakabidhiwa ripoti ya benchi la ufundi na kufanyia kazi kwa kufanya maboresho na msimu ujao tunatarajia kuwa imara," alisema Saido.

# Michezo

Jumapili Juni 11, 2023

Nipashe




UK. 21

## Pogba kutimkia Uarabuni




Msafara wa wachezaji wa timu ya Yanga, ukisindikizwa na mashabiki wa timu hiyo baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jana kutokea jijini Mbeya wakiwa na Kombe lao la Ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mapokezi ya Yanga balaa

### ●●● Mashabiki wafurika kulishuhudia kombe lao, wajipanga kwa fainali FA...

**Na Shufaa Lyimo**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/2023 timu ya Yanga jana Jumamosi walipokelewa kishujaa jijini Dar es Salaam na mashabiki wao wakiwa wanatokea Mbeya walipokuwa wamekwenda kukamilisha mechi zao mbili za mwisho dhidi ya Mbeya City na Prison pamoja na kukabidhiwa kombe lao la ubingwa.

Yanga imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu kufanya vema kwenye michezo yake yote ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na kujikusanyia pointi 78 ikifuatiwa na Simba iliyomaliza na pointi 73.

Kikosi cha Yanga jana kiliwasili uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere majira ya saa 6:00 mchana.

**Mara baada ya kuwasili wachezaji na viongozi walipanda na kombe kwenye gari la wazi na kupita mitaa ya jiji la Dar es Salaam kuelekea makao makuu Jang wani wakipita barabara ya Nyerere na Msimba zi, hali iliyosababisha usafiri wa umma kusi mama kwa muda wa masaa mawili.**

Mashabiki walitanda barabarani wakiwa na furaha ya kuliona kombe ambalo msimu huu limekuwa tofauti na lile la msimu uliopita huku wengi wakitembea kwa miguu kutoka uwanja wa Ndege hadi Makao makuu.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuwasili jijini Dar es Salaam Kocha Msaidizi wa Klabu ya Yanga, Cedrick Kaze alisema wamefurahi kupata ubingwa huo na kudai kazi haikuwa rahisi.

"Tumefurahi kupata kombe hili kwa mara nyingine wachezaji wetu wamepambana kuhakikisha tumepata kombe hili," alisema Kaze.

Alisema anawashukuru mashabiki wao kwani hawakukata tamaa waliwapa ushirikiano tangu Ligi Kuu inaanza hadi sasa.

Rais wa Klabu hiyo, Hersi Said alisema wamefurahi kutwaa kombe hilo na kuwapongeza wachezaji, viongozi pamoja na benchi la ufundi kwa kazi kubwa waliyoifanya.

"Ninawapongeza wachezaji wetu benchi la ufundi kwani wamefanya kazi kubwa hadi leo tumepata kombe hili kwa mara nyingine," alisema Said.

Rais huyo alisema baada ya ubingwa huo kwa sasa wanajipanga kwa ajili ya mchezo wao wa Fainali wa Kombe la FA ambapo watacheza na Azam FC kwenye uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga kesho Jumatatu.

## Mgunda: Tutalipa deni msimu ujao

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda amesema wamekaa na kocha Mkuu, Roberto Robertinho, ili kufanya tathimini ya msimu uliomalizika juzi na kukabidhi mapendekezo yao kwa uongozi kuhakikisha wanalipa deni la mashabiki kwa msimu wa mashindano wa 2022/23.

Simba msimu huu haijatwaa taji lolote na iliishia hatua ya robo fainali kwenye michuano ya kombe la Ligi ya Mabingwa Afrika.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042